# KUMFANYIA ADABU MTUME WA MWENYEZI MUNGU

Kimeandaliwa na:

**Dkt. Muhammad Mukhtari Juma**

Waziri wa Waqfu.

Na Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Kiislamu.

Na mjumbe wa jopo la utafiti wa Kiislamu

Kimetafasiriwa Na:

Prof: Ayman Al-Asar.

Na

Mwl: Fadhili Mansour Swalehe

1444 H - 2022 .

Shirika Kuu la Vitabu la Misri

Shirika Kuu la Vitabu la Misri

Mkurugenzi Mkuu.
Dr. Ahmed Bahi ElDin

# KUMFANYIA ADABU MTUME WA MWENYEZI MUNGU

Kimetafasiriwa na:

**DR. MOHAMMAD MUKHTAR JUMA**
**WAZIRI WA WAQFU**

Chapa ya kwanza
Shirikika Kuu la Vitabu la Misri 2021. S.L.P235 Ramsis 1194 Kornesh Nail – Ramlatu Bolaq Cairo.
Namba ya Post: 11794.
Simu: 202257775109 ndani 149 Fax: 20225764276.

Uchapishaji na utekelezaji
Kituo cha uchapishaji Shirika kuu la Vitabu nchini Misri

Mitazamo iliyopo ndani ya kitabu si msimamo wa shirika bali ni msimamo wa mtunzi kwa hatua ya kwanza.

Haki ya uchapishaji inalindwa na Shirika Kuu la vitabu la Misri. Ni marufuku kuchapisha au kusambaza au kutoa kopi au kuiga kwa hali yeyote ile isipokuwa kwa ruhusa ya Shirika Kuu la Vitabu la Misri au kwa maelekezo ya pande husika.

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

﴿لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ الله أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُو الله وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ الله كَثِيرً﴾

**﴿Hakika nyinyi mnacho kigezo njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtarajia Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu kwa wingi﴾** (l-Ahzaab: 21)

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

# **Utangulizi**.

Shukrani njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mlezi wa viumbe vyote, rehma na amani zimwendee mbora wa wana wa Adam, muombezi pekee na pekee wa kukubaliwa maombi, timilizo la Manabii na Mitume, naye ni Mtume Muhammad Ibn Abdillah pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na mwenye kufuata uongofu wake ziendelee kuwashukia mpaka siku ya Malipo.

## **Baada ya Utangulizi:**

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameutakasa ulimi wa Mtume wetu S.A.W na Akasema: **وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ** ﴿**Hatamki kwa matamanio binafsi**﴾ na aka-

tasa moyo wake S.A.W na Akasema: مَا كَذَبَ الْفُؤَادُ ﴿**Moyo haukusema uwongo uliyo yaona**﴾ na akayatakasa macho yake S.A.W na Akasema: مَا رَأَى ﴿مَا زَاغَ الْبَصَرُ وَمَا طَغَى **Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka**﴾, akaitakasa akili yake S.A.W na Akasema: مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَى ﴿**Mwenzenu huyu hakupotea, wala hakukosea**﴾kisha akamtakasa mwalimu wake S.A.W: عَلَّمَهُ شَدِيدُ الْقُوَى ﴿**Amemfundisha aliye mwingi wa nguvu**﴾ akatakasa tabia zake S.A.W na Akasema: وَإِنَّكَ لَعَلَى خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿**Hakika wewe una tabia tukufu**﴾.

Mola wake Mtukufu alimkunjua kifua chake S.A.W na Akasema: أَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ ﴿**Hatukukunjulia kifua chako?**﴾na akainua utajo wake S.A.W: وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ ﴿**Na tukakunyanyulia utajo wako**﴾ kisha Mwenyezi Mungu akamsamehe makosa yaliyotangulia na yajayo Akasema:

**﴿إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحاً مُّبِينا * لِيَغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ وَيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ وَيَهْدِيَكَ صِرَاطاً مُّسْتَقِيمًا﴾**

**﴿Hakika tumekufungulia Ushindi wa wazi * Ili Mwenyezi Mungu akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yajayo, na akutimizie neema zake, na akuongoe katika Njia Iliyo Nyooka﴾.**

Na akamtakasa na mambo yote kwa kusema:

﴿لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُو اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا.

**﴿Hakika nyinyi mnacho kigezo njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtarajia Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu kwa wingi﴾.**

Na akaupa heshima Umma wake kwa ajili yake S.A.W Akasema:

﴿وَمَا كَانَ اللّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ وَأَنتَ فِيهِمْ وَمَا كَانَ اللّهُ مُعَذِّبَهُمْ وَهُمْ يَسْتَغْفِرُونَ﴾.

**﴿Mwenyezi Mungu hakuwa Mwenye kuwaadhibu na hali wewe ukiwa nao, na wala**

**hakuwa Mwenyezi Mungu Mwenye kuwaadhibu hali ya kuwa wanaomba msamaha﴾.**

Mola wake Mtukufu akampa rehma na Malaika wanamuombea rehma pamoja na Waumini, akasema Mola Mtukufu:

﴿إِنَّ اللَّهَ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا﴾ .

**﴿Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu﴾**. Mola wake amemleta ili kuwa ni rehma kwa walimwengu wote, akasema:

﴿وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ﴾ .

**﴿Wala hatukukupeleka isipokuwa uwe ni rehma kwa walimwengu wote﴾**. Kisha Mwenyezi Mungu akatuamrisha kumfuata Mtume S.A.W akasema:

﴿وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا﴾ .

﴿**Na aliyokuleteeni Mtume basi yachukuweni na yale aliyokukatazeni kwayo basi yaacheni**﴾. Na Mwenyezi Mungu akatutahadharisha na vitendo vya kwenda kinyume na amri zake Mtume S.A.W akasema:

﴿فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ﴾ .

﴿**Na wajihadhari wale ambao wanakwenda kinyume na amri za Mtume watakujafikwa na fitna au kufikwa na adhabu kali**﴾. Na akatukataza kumuita Mtume S.A.W kama tunavyoitana sisi kwa sisi akasema Mola Mtukufu:

﴿لا تَجْعَلُوا دُعَاء الرَّسُولِ بَيْنَكُمْ كَدُعَاء بَعْضِكُم بَعْضًا﴾ .

﴿**Wala musimuite Mtume kati yenu kama vile munavyoitana nyinyi kwa nyinyi**﴾. Kisha Mwenyezi Mungu akaunganisha imani yetu kwa kufuata hukumu zake Mtume S.A.W akasema Mola Mtukufu:

﴿فَلاَ وَرَبِّكَ لاَ يُؤْمِنُونَ حَتَّىَ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لاَ يَجِدُواْ فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجاً مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُواْ تَسْلِيمًا﴾.

**﴿La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayotofautiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenyekee kabisa﴾**.

Mola wetu Mtukufu akafanya utiifu kwa Mtume S.A.W ni katika kumtii Yeye Mola Mtukufu, akasema:

﴿مَّنْ يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللّهَ وَمَن تَوَلَّى فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا﴾.

**﴿Mwenye kumtii Mtume basi ndio amemtii Mwenyezi Mungu. Na anaye kengeuka, basi Sisi hatukukutuma wewe uwe ni mlinzi wao﴾**.

Na akasema tena Mola Mtukufu: **﴿وَمَن يُطِعْ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا﴾** **﴿Mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi huyo atakuwa amefuzu kufuzu kukubwa﴾**. Na akasema

Mola Mtukufu: ﴿وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلالاً مُّبِينًا﴾ **Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi atakuwa amepotea upotevu mkubwa**.

Kutokana na hayo imelazimishwa kujipamba kwa viwango vya juu vya adabu kwa Mtume S.A.W pamoja na kwenye Sunna zake Takatifu na kwenye Msikiti wake Mtukufu, kwani utukufu wake Mtume S.A.W akiwa amefariki ni sawa sawa na utukufu wake alipokuwa hai.

Kufanya adabu kwa Mtume S.A.W ni pamoja na kutotaja jina lake S.A.W likiwa limeepukana na yanayoendana na wasifu wa Utume au Ujumbe au kumtakia rehma na amani, ni sawa sawa wakati wa kumtaja Yeye Mtume S.A.W au kusikia likitajwa jina lake S.A.W au kuandikwa jina lake takatifu S.A.W kwa idadi yeyote itakayoandikwa jina lake au kutajwa.

Kama tunavyosisitiza kuwa kumpenda Mtume wetu Muhammad S.A.W ni sehemu isiyogawa-

nyika na Imani yetu, na kumpenda huko ni sharti katika masharti ya kufaa kwa Imani, ambapo anasema Mtume S.A.W katika Hadithi yake:

**لا يُؤْمِنُ أحدُكم حتى أكونَ أحبَّ إليه من ولدِهِ ، ووالدِهِ ، والناسِ أجمعينَ» .**

"Hawi na imani mmoja wenu mpaka mimi niwe mwenye kupendwa zaidi kwake kuliko watoto wake wazazi wake na watu wote".

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu aturuzuku upendo kwake Mola Mtukufu na atupe upendo kwa Mtume wake S.A.W na atujaalie upendo wa kila mwenye kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mioyo yetu aijaze upendo huu, na aturuzuku ufahamu mzuri wa Kitabu chake na Sunna za Mtume wake, na wala asitunyime uombezi wa Mustafa S.A.W siku ya Kiyama, na atunyweshe kwenye birika kwa mkono wake mtakatifu S.A.W kinywaji chenye utulivu bila ya kupata kiu kabisa, na atustareheshe kwa usikivu wetu na macho yetu na nguvu zetu na aturuzuku

kauli ya kweli katika maisha yetu, na aturuzuku pia usafi wa nia na maadili mema yatakayopelekea maombi yetu kwake Mola Mtukufu ni kwa hali zetu zaidi kuliko maneno, na atufishe akiwa Yu radhi na sisi, na atuwezeshe kufanya matendo mema yatakayo tupelekea mwisho mwema, na atuingize Peponi bila ya kuhesabiwa wala kutanguliwa na adhabu, na awafanyie huruma duniani wanyonge wetu na atustiri na aibu zetu, na atupendezeshe kwa ukarimu wake na stara yake, na wala asitufedheheshe mbele za watu si duniani wala siku ya Akhera, na atuchukulie kwa ukaribu wake na si kwa dhambi zetu na mapungufu yetu, na azitakase nafsi zetu kutokana na ubahiri, na nyoyo zetu kutokana na mazonge, na ajaaliye Msikiti wake Mtakatifu na Msikiti wa Mtume wake S.A.W kuwe ni wenye kufanya ibada ya Umra kwa amani mpaka siku ya Kiyama, na wala asitunyime heshima ya kuswali kwenye Misikiti hiyo kwa kiasi anavyojua namna nafsi zilivyofungamana na upendo Kwake na kwa Mtume wake S.A.W na wala asitufitinishe sisi wenyewe na kwa nafsi zetu,

kwani Yeye Mola Mtukufu ni mwingi wa fadhila na ukarimu, na Mwenye msaada na usaidizi, na Msimamizi wa neema, Yeye ndiyo Mola wetu ni Mola Mwenye neema na Yeye ndio neema ya mwisho wetu.

Mwenyezi Mungu yupo nyuma ya makusudio na Yeye ndiyo toshelezo letu na mbora wa kutegemewa….

Kwake nimetegemea na kwake naegemeza.

***Dkt Muhammad Mukhtari Juma Mabrouk.***

*Waziri wa Waqfu.*

*Mwenyekiti Baraza kuu la mambo ya Kiislamu.*

*Na mjumbe jopo la utafiti wa mambo ya Kiislamu*

*Ndani ya*

*Al-Azhar Al-Sharif.*

# UTAFITI WA KWANZA
## Mazungumzo ya Quran kuhusu Mtume S.A.W

Quran Tukufu imezungumza kuhusu Mtume S.A.W maelezo yenye kuonesha nafasi yake pamoja na tabia zake na mengi kwa upande wa maisha yake, yeye ni Mtume wa huruma ambapo Mola Mtukufu Anasema: وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ

﴿**Wala hatukukupeleka isipokuwa uwe ni rehma kwa walimwengu**﴾[1]. Na Mola Mtukufu Anasema:

﴿فَبِمَا رَحْمَةٍ مِنَ اللَّهِ لِنْتَ لَهُمْ وَلَوْ كُنْتَ فَظًّا غَلِيظَ الْقَلْبِ لَانْفَضُّوا مِنْ حَوْلِكَ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ وَشَاوِرْهُمْ فِي الْأَمْرِ فَإِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَوَكِّلِينَ﴾.

﴿**Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao.**

(1) Al-Ambiyaa: 107.

**Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia. Basi wasamehe, na waombee msamaha, na shauriana nao katika mambo. Na ukisha kata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao mtegemea﴾**(1).

**Na Mola Mtukufu Anasema:**

**﴿لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِنْ أَنْفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ﴾.**

**﴿Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma﴾**(2).

**Na Anasema tena:**

**﴿وَاعْلَمُوا أَنَّ فِيكُمْ رَسُولَ اللَّهِ لَوْ يُطِيعُكُمْ فِي كَثِيرٍ مِنَ الْأَمْرِ لَعَنِتُّمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ حَبَّبَ إِلَيْكُمُ الْإِيمَانَ وَزَيَّنَهُ فِي قُلُوبِكُمْ وَكَرَّهَ إِلَيْكُمُ الْكُفْرَ وَالْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ أُولَئِكَ هُمُ الرَّاشِدُونَ﴾.**

---

(1) Aal-Imraan: 159
(2) At-Tawbah: 128.

**﴿Na jueni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu yuko nanyi. Lau angeli kutiini katika mambo mengi, bila ya shaka mngeli taabika. Lakini Mwenyezi Mungu amekupendezeeni Imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na amekufanyeni muuchukie ukafiri, na upotovu, na uasi. Hao ndio walioongoka﴾**(1).

Na Mtume S.A.W alisema kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusu Nabii Ibrahim:

**﴿رَبِّ إِنَّهُنَّ أَضْلَلْنَ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ فَمَن تَبِعَنِي فَإِنَّهُ مِنِّي وَمَنْ عَصَانِي فَإِنَّكَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾.**

**﴿Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika hayo yamewapoteza watu wengi. Basi aliye nifuata mimi huyo ni wangu, na aliye niasi, hakika Wewe ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu﴾**(2).

Na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kupitia ulimi wa Nabii Isa Amani ya Mungu iwe kwake:

---

(1) Hujraat: 07
(2) Ibrahimu: 36

﴿إِنْ تُعَذِّبْهُمْ فَإِنَّهُمْ عِبَادُكَ وَإِنْ تَغْفِرْ لَهُمْ فَإِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ﴾.

**﴿Ukiwaadhibu basi hao ni waja wako. Na ukiwasamehe basi Wewe ndiye Mwenye nguvu na Mwenye hekima﴾**[1], hivyo akainua mikono yake na akasema: Ewe Mola uma wangu uma wangu na akalia, ndipo Mwenyezi Mungu Mtukufu Akasema: Ewe Jabril, nenda kwa Muhammad na - Mola wako Anajua zaidi – muulize nini kinakuliza, ndipo Malaika Jabril amani ya Mungu iwe kwake akaja na kumuuliza, akampa habari Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa yale aliyoyasema, Naye Anajua zaidi. Mwenyezi Mungu Akasema: Ewe Jibril nenda kwa Muhammad na mwambie: Sisi tutakuridhia kwenye uma wako wala hatutakufanyia ubaya [2].

(1) Maidah: 118

(2) Imo kwenye sahihi ya Imamu Muslimu, kitabu cha Imani, mlango wa maombi ya Mtume S.A.W kwa uma wake. Na kulia kwake kwa kuwaonea huruma, Hadithi nambari 520, na sahihi ya Ibn Habban, kitabu cha maelezo yake Mtume S.A.W kuhusu wema wa Maswahaba R.A, utajo wa msamaha wa

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameutakasa ulimi wa Mtume wake S.A.W na Akasema: ﴿**وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوَى**﴾[1] ﴿**Wala hazungumzi kwa matamanio**﴾, akatakasa moyo wake na Akasema: ﴿**مَا كَذَبَ الْفُؤَادُ مَا رَأَى**﴾ ﴿**Moyo haukusema uwongo uliyo yaon**a﴾[2], akamtasa Mwalimu wake na Akasema: ﴿**عَلَّمَهُ شَدِيدُ الْقُوَى**﴾ ﴿**Amemfundisha aliye mwingi wa nguvu**﴾[3]. Na akatakasa tabia zake akasema:

﴿**وَإِنَّكَ لَعَلَى خُلُقٍ عَظِيمٍ**﴾ ﴿Hakika wewe una tabia tukufu﴾[4]. Akakifungua kifua chake akasema: ﴿**أَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ**﴾ ﴿**Hatukukunjulia kifua chako**﴾[5]. Na akaunyanyua utajo wake akasema: ﴿**وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ**﴾ ﴿**Na tukakunyanyulia utajo wako**﴾[6].

---

Mwenyezi Mungu Mtukufu dhambi za Bibi Aisha zilizotangulia na zitakazo kuja, Hadithi nambari 7111.

(1) An-Najmu: 3
(2) An-Naimu: 11
(3) An-Najmu: 5
(4) Al-Qalam: 4
(5) As-Sharhu: 1
(6) As-Sharhu: 4.

Na akamsamehe makosa yake yaliyotangulia na yatakayo kuja akasema:

﴿إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُبِينًا * لِيَغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ﴾.

**﴿Hakika tumekufungulia Ushindi wa wazi * Ili Mwenyezi Mungu akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yajayo, na akutimizie neema zake, na akuongoe katika Njia Iliyo Nyooka﴾**[1].

Mola wake akamkirimu hata katika kuzungumza naye na kumuita kwake, ambapo Mola Mtukufu aliwaita Manabii kwa majina yao: **يَا آدَمُ اسْكُنْ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ ﴿Ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani﴾**[2].

﴿يَا نُوحُ اهْبِطْ بِسَلَامٍ مِنَّا وَبَرَكَاتٍ عَلَيْكَ وَعَلَى أُمَمٍ مِمَّنْ مَعَكَ﴾.

**﴿Ikasemwa: Ewe Nuhu! Shuka kwa salama itokayo kwetu, na baraka nyingi juu yako na juu ya watu waliopamoja nawe﴾**[3].

(1) Al-Fat'hi: 1, 2
(2) Al-Baqarah: 35 na Al-Aaraf: 13.
(3) Huud: 48

﴿يَا إِبْرَاهِيمُ قَدْ صَدَّقْتَ الرُّؤْيَا إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ﴾.

**﴿Ewe ibrahim Umekwisha itimiliza ndoto. Hakika hivi ndivyo tunavyo walipa wanao tenda mema﴾**[1]. ﴿إِنَّا جَعَلْنَاكَ خَلِيفَةً فِي الْأَرْضِ فَاحْكُم بَيْنَ النَّاسِ بِالْحَقِّ يَا دَاوُودُ﴾ **﴿Ewe Daudi! Hakika Sisi tumekufanya wewe uwe kiongozi katika nchi﴾**[2]. ﴿يَا زَكَرِيَّا إِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلَامٍ اسْمُهُ يَحْيَى﴾ **﴿Ewe Zakariya! Hakika Sisi tunakubashiria mwana; jina lake ni Yahya﴾**[3]:

﴿يَا يَحْيَى خُذِ الْكِتَابَ بِقُوَّةٍ﴾.

**﴿Ewe Yahya! Kishike Kitabu kwa nguvu!﴾**[4].

﴿يَا مُوسَى إِنِّي أَنَا رَبُّكَ فَاخْلَعْ نَعْلَيْكَ إِنَّكَ بِالْوَادِ الْمُقَدَّسِ طُوًى﴾.

**﴿Ewe Musa Hakika Mimi ndiye Mola wako Mlezi! Basi vua viatu vyako. Kwani upo katika**

(1) Swaafaat: 105.
(2) Swaad: 26
(3) Maryam: 7
(4) Maryma: 12

**bonde takatifu la Tuwa﴿(1). ﴿يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ اذْكُرْ نِعْمَتِي عَلَيْكَ وَعَلى وَالِدَتِكَ﴾ Ewe Isa Ibn Maryamu! Kumbuka neema yangu juu yako, na juu ya mama yako﴾**(2).

Akazungumza na Mtume Muhammad S.A.W mazungumzo yaliyoambatana na heshima ya Ujumbe au Utume, au sifa kumkirimu kumfadhilisha na upole, Mola Mtukufu Akasema: **﴿يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ﴾ ﴿Ewe Mtume! Fikisha uliyo teremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi﴾**(3).

**﴿يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ شَاهِدًا وَمُبَشِّرًا وَنَذِيرًا﴾.**

**﴿Ewe Nabii! Hakika Sisi tumekutuma uwe shahidi na mbashiri na mwonyaji﴾**(4).

**﴿يَا أَيُّهَا الْمُزَّمِّلُ قُمِ اللَّيْلَ إِلَّا قَلِيلًا﴾.**

---

(1) Twaha: 12
(2) Maidah: 110.
(3) Maidah: 67
(4) Ahzaab: 45

﴿**Ewe uliye jifunika * Kesha usiku kucha, ila kidogo tu**﴾[1]. ﴿يَاأَيُّهَا الْمُدَّثِّرُ قُمْ فَأَنْذِرْ﴾ **Ewe uliye jigubika! * Simama uonye**﴾[2]. Na pindi Mwenyezi Mungu alipolitaja jina lake ndani ya Quran Tukufu alilitaja kwa kukutanisha na nguvu ya Ujumbe, akasema Mola Mtukufu: ﴿مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءُ بَيْنَهُمْ﴾ ﴿**Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na waliopamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao**﴾[3]. ﴿وَمَا مُحَمَّدٌ إِلاَّ رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ﴾ ﴿**Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwishapita kabla yake Mitume**﴾[4]. ﴿مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَكِن رَّسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ﴾ ﴿**Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii**﴾[5]. Akachukuwa ahadi

(1) Al-Muzzammil: 1, 2
(2) Al-Muddaththir: 1, 2
(3) Fat'hi: 29
(4) Aal-Imran: 144.
(5) Ahzaab: 40

kwa Manabii na Mitume kuwa watamuamini na kumtetea, akasema Mola Mtukufu:

﴿وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ النَّبِيِّينَ لَمَا آتَيْتُكُمْ مِنْ كِتَابٍ وَحِكْمَةٍ ثُمَّ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مُصَدِّقٌ لِمَا مَعَكُمْ لَتُؤْمِنُنَّ بِهِ وَلَتَنْصُرُنَّهُ قَالَ أَأَقْرَرْتُمْ وَأَخَذْتُمْ عَلَى ذَلِكُمْ إِصْرِي قَالُوا أَقْرَرْنَا قَالَ فَاشْهَدُوا وَأَنَا مَعَكُمْ مِنَ الشَّاهِدِينَ﴾.

**﴿Na pale Mwenyezi Mungu alipo chukua ahadi kwa Manabii: Nikisha kupeni Kitabu na hekima, kisha akakujieni Mtume mwenye kusadikisha mliyo nayo, ni juu yenu mumuamini na mumsaidie. Akasema: Je, mmekiri na mmekubali kushika agizo langu juu ya hayo? Wakasema: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika kushuhudia﴾**(1).

Mwenyezi Mungu akakutanisha kumtii Mtume S.A.W na utiifu wake, Mola Mtukufu Akasema: ﴿مَنْ يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللهَّ﴾ **﴿Mwenye kumtii Mtume basi ndio amemtii Mwenyezi Mungu﴾**(2).

(1) Aal-Imraan: 81
(2) An-Nisaa: 80.

**Akaendelea tena kusema Mola Mtukufu:**

**﴿وَمَنْ يُطِعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ وَحَسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا﴾.**

**﴿Na menye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wapamoja na wale alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!﴾**[1].

Kisha Mwenyezi Mungu akafanya upendo kwake S.A.W njia ya upendo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, akasema Mola Mtukufu:

**﴿قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾.**

**﴿Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu**

(1) An-Nisaa: 69.

**atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu﴾**[1]. Akafanya kiapo cha utiifu kwa Mtume S.A.W ni kiapo cha utiifu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّ الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّهَ يَدُ اللَّهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ﴾.

**﴿Bila ya shaka wanao fungamana nawe, kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao﴾**[2].

Na Abdillah Ibn Abbas R.A alikuwa anasema: Kuna Aya tatu zimeteremka zikikutana na Aya tatu haikubaliki moja kati ya hizo bila ya kuwa na mwenza wake, Aya ya kwanza: **وَأَقِيمُوا الصَّلاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ** **﴿Na shikeni Sala na toeni Zaka﴾**(3). Aya ya pili kauli yake Mola Mtukufu: **أن اشْكُرْ لِي وَلِوَالِدَيْكَ**

(1) Aal-Imran: 41.
(2) Fat'h: 10.
(3) Al-Baqarah: 43



الأدب مع سيدنا رسول الله باللغة السواحيلي

**Nishukuru Mimi na wazazi wako**﴾[1]. Na Aya ya tatu ni kauli yake Mola Mtukufu: **وَأَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ** ﴿**Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume**﴾[2]. Mwenye kumtii Mwenyezi Mungu bila ya kumtii Mtume utiifu wake hautokubalika [3].

Mwenyezi Mungu Mtukufu Ametahadharisha na kwenda kinyume na amri za Mtume S.A.W akasema: **فَلْيَحْذَرِ ٱلَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِۦٓ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ** ﴿**Basi nawatahadhari wanao kwenda kinyume na amri yake, usije ukawapata msiba au ikawapata adhabu chungu**﴾[4]. Akisisitiza kuwa kumuamini Mtume S.A.W hakukamiliki isipokuwa kwa kufuata hukumu zake kwa kuridhia na kwa nafsi njema, akasema Mola Mtukufu:

---

(1) Luqman: 14
(2) An-Nisaa: 59
(3) Kitabu cha sehemu za Imani cha Imamu Baihaqy, inasehemu hamsini na tano, mlango wa kuwafanyiawema wazazi wawili. Hadihi nambari 7830 chapa ya Dar Al-Kutub Al-Ilmiyah ya Beiruti.
(4) An-Nuur: 63.

﴿فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّى يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنْفُسِهِمْ حَرَجًا مِمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا﴾.

**﴿La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayotafautiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenyekee kabisa﴾**[1]. Na Mwenyezi Mungu akakataza kuinua sauti mbele ya Mtume S.A.W akasema Mola Mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَنْ تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تَشْعُرُونَ إِنَّ الَّذِينَ يَغُضُّونَ أَصْوَاتَهُمْ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ أُولَئِكَ الَّذِينَ امْتَحَنَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ لِلتَّقْوَى لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ﴾.

**﴿Enyi mlio amini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Mtume, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui * Kwa hakika wanao teremsha sauti**

(1) An-Nisaa: 65.

**zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio Mwenyezi Mungu amezisafisha nyoyo zao kwa ucha-Mungu. Hao watakuwa na msamaha na malipo makubwa﴾**[1]. Imamu Maliki Mungu amrehemu alimsikia mtu mmoja akinyanyua sauti yake ndani ya Msikiti wa Mtume S.A.W akasema: Ewe unayefanya haya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwakemea watu na akasema:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَنْ تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تَشْعُرُونَ﴾.

**﴿Enyi mlio amini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Mtume, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui﴾**[2]. Na akawasifu watu kwa kusema:

﴿إِنَّ الَّذِينَ يَغُضُّونَ أَصْوَاتَهُمْ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ أُولَئِكَ الَّذِينَ امْتَحَنَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ لِلتَّقْوَى لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ﴾.

(1) Al-Hujraat: 2, 3
(2) Al-Huraat: 2

﴿**Kwa hakika wanao teremsha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio Mwenyezi Mungu amezisafisha nyoyo zao kwa ucha-Mungu. Hao watakuwa na msamaha na malipo makubwa**﴾(1). Na heshima ya Mtume S.A.W akiwa amefariki ni sawa sawa na heshima yake wakati wa uhai, hivyo kuwa na adabu ndani ya Msikiti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W.

Na katika heshima ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa Mtume wake S.A.W ni kuufanya Ujumbe wake kuwa ni kwa watu wote, ambapo ilikuwa kila Mtume anapelekwa kwa watu wake maalum, ama Mtume wetu Muhammad S.A.W amepelekwa na Mola wake kwa watu wote, akasema Mola Mtukufu:

﴿**وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَّةً لِلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا**﴾.

﴿**Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri, na mwonyaji**﴾(2). Na kuufanya Ujumbe

(1) Al-Hujraat: 3
(2) Sabai: 28

wake kuwa ndio Ujumbe wa mwisho, na kumfanya Mtume S.A.W kuwa ndio hitimisho la Manabii na Mitume, akasema Mola Mtukufu:

﴿مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِنْ رِجَالِكُمْ وَلَكِنْ رَسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ﴾.

**﴿Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii﴾**(1). Mwenyezi Mungu amemteremshia rehma zake na akawaamrisha Malaika wake na Waumini kumtakia rehma, akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا﴾.

**﴿Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Mtume. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu﴾**(2). Mwenyezi Mungu akafanya maombi yake Mtume kwa Waumini ni

(1) Al-Ahzaab: 40
(2) Al-Ahzaab: 56

rehma na utulivu kwao, akasema Mola Mtukufu: **﴿Na وَصَلِّ عَلَيْهِمْ إِنَّ صَلَاتَكَ سَكَنٌ لَّهُمْ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيم uwaombee rehema. Hakika maombiyako ni utulivu kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua﴾**[1].

Hivyo ni juu yetu kufanya wingi wa kumtakia rehma na amani Mtume S.A.W kwani mwenye kumtakia rehma mara moja basi anamalipo ya thawabu kumi, kama vile kumtakia kwetu rehma huwa kunafikishwa kwake Mtume S.A.W na Mtume alikuwa anasema:

**﴿إِذا سمِعْتُمُ النِّداءَ فَقُولُوا مِثْلَ ما يَقُولُ ، ثُمَّ صَلُّوا عليَّ ، فَإِنَّهُ مَنْ صَلَّى علَيَّ صَلاةً صَلَّى اللَّه عَلَيْهِ بِهَا عشْرًا ، ثُمَّ سلُوا اللَّه لي الْوسِيلَةَ ، فَإِنَّهَا مَنزِلَةٌ في الجنَّةِ لا تَنْبَغِي إِلاَّ لعَبْدٍ من عِباد اللَّه وَأَرْجُو أَنْ أَكُونَ أَنَا هُو ، فمَنْ سَأَل لِيَ الْوسِيلَةَ حَلَّتْ لَهُ الشَّفاعَةُ﴾ .**

"Pindi munaposikia adhana basi semeni kama anavyosema muadhini, kisha munitakie rehma, kwani mwenye kunitakia rehma mara moja ana

(1) At-Taubah: 103.

thawabu kumi, kisha niombeeni kwa Mwenyezi Mungu Al-Wasiilah, kwani hiyo Wasiilah ni nafasi ya juu Peponi ambayo hapaswi kuwepo hapo isipokuwa mja katika waja wa Mwenyezi Mungu na mimi nategemea kuwa ni mimi, basi mwenye kuniombea Al-Wasiilah huyo amehalalikiwa na maombezi" (1).

(1) Ni Hadithi iliyokubaliwa na wapokezi wote, inapatikana kwenye sahihi Muslimu na sahihi Bukhary, kitabu cha adhana mlango wa anayoyasema pindi anapomsikia muadhini. Hadithi nambari 611, na katika sahihi Muslimu, kitabu cha swala mlango wa Sunna kusema mfano wa kauli ya muadhini kwa mwenye kumsikia kisha akamtakia rehma Mtume S.A.W kisha akamuomba Mwenyezi Mungu Al-Wasiilah. Ni Hadithi nambari 875.

## UTAFITI WA PILI.

## Umuhimu wa Sunna Takatifu na nafasi yake katika utungaji Sharia.

Pindi tunapozungumza kuhusu Sunna Takatifu za Mtume S.A.W basi tunazungumzia chanzo cha pili cha utungaji Sharia, Wanachuoni wa Umma wamekubaliana juu ya umuhimu wa Sunna za Mtume, na kumtii Mtume S.A.W ni katika kumtii Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا الله وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنكُمْ فَإِن تَنَازَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى الله وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِالله وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا﴾.

**﴿Enyi mlio amini! Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi. Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume,**

**ikiwa mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hayo ndiyo bora zaidi na ndiyo yenye mwisho mwema﴾**[1]. Na Anasema tena Mola Mtukufu: ﴿وَأَطِيعُوا اللهَ وَالرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ﴾. **﴿Na mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume ili mpate kurehemewa﴾**[2].

Na Anasema Mola Mtukufu:

﴿قُلْ أَطِيعُوا الله وَالرَّسُولَ فَإِن تَوَلَّـوْا فَإِنَّ الله لَا يُحِبُّ الْكَافِرِينَ﴾.

**﴿Sema: Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume. Na wakigeuka basi Mwenyezi Mungu hawapendi makafiri﴾**[3]. Na Anasema Mola Mtukufu:

﴿وَأَطِيعُوا الله وَرَسُولَهُ وَلَا تَنَازَعُوا فَتَفْشَلُوا وَتَذْهَبَ رِيحُكُمْ وَاصْبِرُوا إِنَّ الله مَعَ الصَّابِرِينَ﴾.

**﴿Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala msizozane mkaingiwa woga, na zikapotea nguvu zenu. Na subirini. Hakika Mwe-**

(1) An-Nisaa: 59
(2) Aal-Imraan: 132.
(3) Aal-Imraan: 32.

**nyezi Mungu yu pamoja na wanao subiri﴾**[1]. Na Anasema tena Mola Mtukufu:

﴿وَأَطِيعُوا الله وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَاحْذَرُوا فَإِن تَوَلَّيْتُمْ فَاعْلَمُوا أَنَّمَا عَلَى رَسُولِنَا الْبَلَاغُ الْمُبِينُ﴾.

**﴿Na mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume, na tahadharini. Na ikiwa mtageuka basi jueni ya kuwa jukumu la Mtume wetu ni kufikisha ujumbe tu ulio wazi﴾**[2]. Na Anaendelea tena kusema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿قُلْ أَطِيعُوا الله وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ فَإِن تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْهِ مَا حُمِّلَ وَعَلَيْكُم مَّا حُمِّلْتُمْ وَإِن تُطِيعُوهُ تَهْتَدُوا وَمَا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا الْبَلَاغُ الْمُبِينُ﴾.

**﴿Sema: Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume. Na mkigeuka, basi jukumu lake ni alilobebeshwa, na jukumu lenu ni mliyobebeshwa nyinyi. Na mkimtii yeye mtaongoka. Na**

(1) Al-Anfaal: 46.
(2) Al-Maidah: 92

**hapana juu ya Mtume ila kufikisha Ujumbe wazi wazi﴾**[1].

Na Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**﴿مَّن يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ الله وَمَن تَوَلَّى فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا﴾.**

**﴿Mwenye kumtii Mtume basi ndio amemtii Mwenyezi Mungu. Na anaye kengeuka, basi Sisi hatukukutuma wewe uwe ni mlinzi wao﴾**[2]. Na Anasema tena Mola Mtukufu:

**﴿وَمَن يُطِعِ الله وَالرَّسُولَ فَأُولَئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ الله عَلَيْهِم مِّنَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ وَحَسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا ذَلِكَ الْفَضْلُ مِنَ الله وَكَفَى بالله عَلِيمًا﴾.**

**﴿Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wapamoja na wale alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii,**

(1) An-Nuur: 54.
(2) An-Nisaa: 80

**na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao! * Hiyo ni fadhila itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kutosha﴾**[1]. Na Anaendelea kusema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَمَن يُطِعِ اللهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا﴾.

**﴿Na anaye mtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, bila ya shaka amefanikiwa mafanikio makubwa﴾**[2]. Na Anasema tena Mola Mtukufu:

﴿تِلْكَ حُدُودُ اللهِ وَمَن يُطِعِ اللهَ وَرَسُولَهُ يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ﴾.

**﴿Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na anaye mtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, Yeye atamtia katika Pepo zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Na huko ndiko kufuzu**

(1) An-Nisaa: 69. 70
(2) Al-Ahzaab: 71.

**kukubwa**﴾[1]. Na Anasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَمَن يُطِعِ الله وَرَسُولَهُ يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَمَن يَتَوَلَّ يُعَذِّبْهُ عَذَابًا أَلِيمًا﴾.

**﴿Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, atamuingiza katika Mabustani yapitayo mito kati yake. Na atakaye geuka upande atamuadhibu kwa adhabu chungu﴾**[2]. Na Anasema Mola Mtukufu:

﴿إِنَّمَا كَانَ قَوْلَ الْمُؤْمِنِينَ إِذَا دُعُوا إِلَى الله وَرَسُولِهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ أَن يَقُولُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ وَمَن يُطِعِ الله وَرَسُولَهُ وَيَخْشَ الله وَيَتَّقْهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَائِزُونَ﴾.

**﴿Haiwi kauli ya Waumini wanapo itwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ili ahukumu baina yao, ila nikusema: Tumesikia, na tumetii! Na hao ndio wenye kufanikiwa * Na wenye**

(1) An-Nisaa: 13.
(2) Al-Fat'hu: 17

**kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakamuogopa Mwenyezi Mungu na wakamcha, basi hao ndio wenye kufuzu﴾**[1]. Na Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**﴿وَمَا أَرْسَلْنَا مِن رَّسُولٍ إِلَّا لِيُطَاعَ بِإِذْنِ الله وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذ ظَّلَمُوا أَنفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا الله وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ لَوَجَدُوا الله تَوَّابًا رَّحِيمًا﴾.**

**﴿Na hatukumtuma Mtume yeyote ila atiiwe kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na lau pale walipo jidhulumu nafsi zao wangelikujia, wakamuomba Mwenyezi Mungu msamaha, na Mtume akawaombea msamaha, hapana shaka wangeli mkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu﴾**[2]. Na Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**﴿وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا وَاتَّقُوا الله إِنَّ الله شَدِيدُ الْعِقَابِ﴾.**

---

(1) An-Nuur: 51, 52
(2) An-Nisaa: 64.

﴿**Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu**﴾[1].

Quran Tukufu inasisitiza umuhimu wa kutafuta hukumu kwa Mtume S.A.W katika uhai wake na kwa muktadha wa Sunna zake Takatifu katika uhai wake na baada ya kufariki kwake, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

﴿فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّى يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا﴾.

﴿**La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayotofautiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenyekee kabisa**﴾[2]. Na Anasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu:

(1) Al-Hashri: 7
(2) An-Nisaa: 65.

﴿وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى الله وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ وَمَن يَعْصِ الله وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا﴾.

**﴿Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na hiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapo kata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi﴾**[1].

Mwenyezi Mungu amekataza na kutahadharisha kwenda kinyume na Mtume S.A.W akasema Mola Mtukufu:

﴿فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَنْ تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ﴾.

**﴿Basi nawatahadhari wanao kwenda kinyume na amri yake, usije ukawapata msiba**

(1) Al-Ahzaab: 36.

**au ikawapata adhabu chungu﴾**[1]. Na Anasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا الله وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَلَا تُبْطِلُوا أَعْمَالَكُمْ﴾.

**﴿Enyi mlio amini! Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume, wala msiviharibu vitendo vyenu﴾**[2]. Anasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا الله وَرَسُولَهُ وَلَا تَوَلَّوْا عَنْهُ وَأَنتُمْ تَسْمَعُونَ * وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ قَالُوا سَمِعْنَا وَهُمْ لَا يَسْمَعُونَ * إِنَّ شَرَّ الدَّوَابِّ عِندَ الله الصُّمُّ الْبُكْمُ الَّذِينَ لَا يَعْقِلُونَ * وَلَوْ عَلِمَ الله فِيهِمْ خَيْرًا لَّأَسْمَعَهُمْ وَلَوْ أَسْمَعَهُمْ لَتَوَلَّوا وَّهُم مُّعْرِضُونَ﴾.

**﴿Enyi mlio amini! Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala msijiepushe naye, nanyi mnasikia * Wala msiwe kama wale wanao sema: Tumesikia, na kumbe hawasikii * Hakika vin-**

(1) An-Nuur: 63.
(2) Muhammad: 33

**yama viovu mbele ya Mwenyezi Mungu ni vile viziwi na bubu visio tumia akili zao * Na Mwenyezi Mungu angelijua wema wowote kwao angewasikilizisha, na lau angewasikilizisha wangeligeuka wakapuuza﴾**[1].

Na Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: **﴿وَمَن يَعْصِ اللهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا﴾ Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi﴾**[2]. Na Anasema tena Mola Mtukufu:

**﴿وَمَن يَعْصِ الله وَرَسُولَهُ وَيَتَعَدَّ حُدُودَهُ يُدْخِلْهُ نَارًا خَالِدًا فِيهَا وَلَهُ عَذَابٌ مُّهِينٌ﴾.**

**﴿Na anaye muasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na akaipindukia mipaka yake, Mwenyezi Mungu atamtia motoni adumu humo, na atapata adhabu ya kudhalilisha﴾**[3].

(1) Al-Anfaal: 20 – 23.
(2) Al-Ahzaab: 36.
(3) An-Nisaa: 14.

**Na Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:**

﴿وَمَن يَعْصِ الله وَرَسُولَهُ فَإِنَّ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا﴾ .

**﴿Na wenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi hakika hao watapata moto wa jahannamu wadumu humo milele﴾**[1].

Na Mwenyezi Mungu Mtukufu anatubainishia kuwa kila maelekezo yanayotolewa na Mtume S.A.W ni ufunuo anaofunuliwa nao, ambapo Mwenyezi Mungu Anasema:

﴿وَالنَّجْمِ إِذَا هَوَى * مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَى * وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوَى * إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَى﴾ .

**﴿Naapa kwa nyota inapo tua * Mwenzenu huyu hakupotea, wala hakukosea * Wala hatamki kwa matamanio * Hayakuwa haya ila ni ufunuo ulio funuliwa﴾**[2]. Naye Mtume S.A.W

(1) Al-Jinni: 23.
(2) An-Najmu: 1 - 4

anatulingania katika yale yanayotupa uzima, ambapo Mwenyezi Mungu Anasema:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لله وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ وَاعْلَمُوا أَنَّ الله يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ﴾.

**﴿Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa﴾**[1].

Na Mwenyezi Mungu Mtukufu amefanya kumtii Mtume S.A.W na kufuata Sunna zake ni sababu ya kupata radhi zake Mola Mtukufu na upendo wake, na ni mlango wa kupata msamaha wa dhambi, Amesema Mola Mtukufu:

﴿قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ الله فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ الله وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَالله غَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾.

(1) Al-Anfaal: 24

**﴿Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu﴾**(1).

**Na anasema Mtume wetu S.A.W:**

**﴿أَلَا هَلْ عَسَى رَجُلٌ يَبْلُغُهُ الحَدِيثُ عَنِّي وَهُوَ مُتَّكِئٌ عَلَى أَرِيكَتِهِ ، فَيَقُولُ : بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ كِتَابُ الله ، فَمَا وَجَدْنَا فِيهِ حَلَالًا اسْتَحْلَلْنَاهُ ، وَمَا وَجَدْنَا فِيهِ حَرَامًا حَرَّمْنَاهُ ، وَإِنَّ مَا حَرَّمَ رَسُولُ الله كَمَا حَرَّمَ الله﴾.**

"Wakati umefika mtu kuwa anazungumza kuhusu Mimi hali amekaa kwenye kitanda chake na anasema: Kinachotutenganisha kati yetu na nyinyi katika mambo ya dini ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, tutakachokuta ndani ya Quran kimehalalishwa tutakihalalisha, na tutakachokuta ndani ya Quran kimeharamishwa tutakiharamisha. Wakati

(1) Aal-Imraan: 31

kilichoharamishwa na Mtume wa Mwenyezi ni kama kimeharamishwa na Mwenyezi Mungu" [1].

**Na anasema tena Mtume S.A.W:**

**دَعُونِي مَا تَرَكْتُكُمْ إِنَّمَا هَلَكَ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ بِسُؤَالِهِمْ وَاخْتِلَافِهِمْ عَلَى أَنْبِيَائِهِمْ، فَإِذَا نَهَيْتُكُمْ عَنْ شَيْءٍ فَاجْتَنِبُوهُ ، وَإِذَا أَمَرْتُكُمْ بِأَمْرٍ فَأْتُوا مِنْهُ مَا اسْتَطَعْتُمْ﴾ .**

"Musiulizie sana katika yale niliyokuachieni, kwani wameangamia waliokuwa kabla yenu kutokana na wingi wa kuuliza kwao na kutafautiana na Manabii wao, pindi nipowakataza kitu basi jiepusheni nacho, na pindi ninapo waamrisheni jambo basi lifanyeni kadiri muwezavyo" [2].

**Na anasema Mtume S.A.W:**

**كُلُّ أُمَّتِي يَدخُلُونَ الجَنَّةَ إلاَّ مَنْ أبى، قيلَ: وَمَنْ يَأبى يا رَسُول الله ؟ قَالَ: «مَنْ أَطَاعَنِي دَخَلَ الجَنَّةَ ، وَمَنْ عَصَانِي فَقَدْ أبى﴾ .**

---

(1) Sunani Tirmidhy, kitabu cha elimu, mlango wa yaliyokatazwa kusemwa kwenye Hadithi ya Mtume SAW. Hadithi nambari 2664.

(2) Sahihi Bukhary, kitabu cha kushikamana na Kitabu pamoja na Hadithi, mlango wa kufuata Sunna za Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW. Hadithi nambari 7288.

“Uma wangu wote utaingia Peponi isipokuwa yule atakayekataa, akaulizwa Mtume ni nani atakayekataa ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: Mwenye kutii mimi ataingia Peponi, na mwenye kuniasi mimi huyo atakuwa amekataa”[1].

Na kutoka kwa Abdillah Ibn Abbas R.A kuwa Mtume S.A.W amesema:

**« تركتُ فيكم أيُّها الناس ما إنِ اعتصمتم به فلن تضلُّوا أبدًا : كتاب الله ، وَسُنَّةَ نَبِيِّهِ.**

“Enyi watu nimekuachieni ambavyo ikiwa mutashikiamana navyo basi hamtapotea kabisa: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume wake” [2].

Kutoka kwa Al-Arbadh Ibn Sariyah R.A amesema kuwa Mtume S.A.W amesema:

(1) Chanzo kilichotangulia, Hadithi nambari 7280.
(2) Kitabu cha Al-Mustadriki cha Imamu Hakim, kitabu cha Elimu. Hadithi nambari 318.

أُوصِيكُمْ بِتَقْوَى الله ، وَالسَّمْعِ وَالطَّاعَةِ، وَإِنْ عَبْدًا حَبَشِيًّا ، فَإِنَّهُ مَنْ يَعِشْ مِنْكُمْ بَعْدِى فَسَيَرَى اخْتِلاَفًا كَثِيرًا؛ فَعَلَيْكُمْ بِسُنَّتِي وَسُنَّةِ الْخُلَفَاءِ الْمَهْدِيِّينَ الرَّاشِدِينَ ، تَمَسَّكُوا بِهَا وَعَضُّوا عَلَيْهَا بِالنَّوَاجِذِ ، وَإِيَّاكُمْ وَمُحْدَثَاتِ الأُمُورِ، فَإِنَّ كُلَّ مُحْدَثَةٍ بِدْعَة ، وَكُلَّ بِدْعَةٍ ضَلاَلَة.

"Nina wausia kumcha-Mungu, usikivu na utiifu kwa viongozi, hata kama kiongozi atakuwa ni Mhabeshi, yeyote atakayeishi miongoni mwenu baada yangu na akaona tafauti nyingi basi ni juu yenu kufuata Sunna zangu na Sunna za Makhalifa waongofu, shikilieni Sunna hizo kwa meno ya magego, na jihadharini na mambo ya kuzushwa, kwani kila chenye kuzushwa ni uzushi, na kila uzushi ni upotovu" (1).

Na anasema Mtume S.A.W: فَمَنْ رَغِبَ عَنْ سُنَّتِي فَلَيْسَ مِنِّي "Mwenye kuachana na mwenendo wangu basi huyo si katika watu wangu" (2).

---

(1) Sunani Abi Daud, kitabu cha Sunna, mlango wa kuwajibika na Sunna. Hadithi nambari 4607.
(2) Imekubaliwa kwenye sahihi Bukhary, kitabu cha mambo ya

Na anasema tena Mtume S.A.W: مَنْ أَطَاعَنِي فَقَدْ أَطَاعَ الله، وَمَنْ عَصَانِي فَقَدْ عَصى الله "Mwenye kunitii mimi atakuwa amemtii Mwenyezi Mungu, na mwenye kuniasi mimi atakuwa amemuasi Mwenyezi Mungu" (1).

Na imenukuliwa na Ibn Rajabu Al-Hambaly(2)

---

ndoa, mlango wa kukana ndoa, Hadithi nambari 5063, na katika sahihi Muslimu kitabu cha ndoa, mlango wa Sunna za ndoa kwa mwenye uwezo wa kumudu mahitaji, hadithi nambari 1401.

(1) Imekubalika kwenye sahihi Bukhary, kitabu cha Hukumu, mlango wa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ﴿Mtiini Mwenyezi Mungu na mumtii Mtume pamoja na wasimamizi wa mambo﴾ Hadithi nambari 7137, na sahihi Muslimu, kitabu cha mambo ya uongozi, mlango wa wajibu wa kutii viongozi katika mambo yasiyokuwa ya maasi, na kuzuiliwa kuwatii katika mambo ya maasi. Hadithi nambari 1835.

(2) Naye ni: Abu Al-Farhu Zainu deen Abdulrahman Ibn Ahmad Ibn Rajabu Assalaamy Al-Bakhdady, anafahamika kwa jina la Ibn Rajabu Al-Hambaly, alizaliwa Baghdad 736H, alihifadhi Hadithi na kufikia kiwango cha Imamu katika fani ya Hadithi ni miongoni mwa wasomi wa madhehebu ya Imamu Hambaly, miongoni mwa vitabu vyake muhimu ni: Jaamii al-Uluumi wal Hikam, Latwaifu Al-Maarifi. Alifariki huko Damascus mwaka 795H.

kutoka kwa Imamu Ahmad Ibn Hambal [1]. Amesema: Asili ya Uislamu ipo kwenye Hadithi tatu: Hadithi ya Omar: إِنَّمَا الْأَعْمَالُ بِالنِّيَّاتِ "Hakika matendo yote yanakwenda kwa nia". Na Hadithi ya Bibi Aisha R.A: مَنْ أَحْدَثَ فِي أَمْرِنَا هَذَا مَا لَيْسَ مِنْهُ فَهُوَ رَدٌّ "Mwenye kuanzisha jambo katika dini yetu ambalo halipo basi jambo hilo linarudishwa". Na Hadithi ya Nuuman Ibn Bashir: الْحَلَالُ بَيِّنٌ وَالْحَرَامُ بَيِّنٌ "Halali ipo wazi na haramu ipo wazi" [2].

Kutoka kwa Abi Daud Sijistany [3] amesema: Fiqhi inazunguka kwenye Hadithi tano: الْحَلَالُ بَيِّنٌ وَالْحَرَامُ بَيِّنٌ "Halali ipo wazi na haramu ipo wazi" na

(1) Ni Abdillah Ahmad Ibn Muhammad Ibn Hambal alizaliwa mwaka 164, ni Imamu wa nne katika Maimamu wa Watu wa Sunna na Jamaa, na mwenye madhehebu ya Hambaly katika fiqhi ya Kiisalmu, alifariki mwaka 241H.

(2) Kitabu Jaamii Al-Uluum wal Hikam cha Ibn Rajabu Al-Hambaly 1/61 chapa ya Dar Al-Maarifah, Beiruti.

(3) Ni Imamu Abu Daudi, Sulaiman Ibn Al-Ashath Ibn Isaka Ibn Bashiri Al-Azdy Sijistany, Imamu wa Wasomi wa Hadithi katika zama zake, asili yake ni kutoka Sijistan, ndio mwenye kitabu cha Sunani nacho ni moja ya vitabu vya Hadithi, alifariki huko Basrah mwaka 275.

kauli yake Mtume S.A.W لَا ضَرَرَ وَلَا ضِرَارَ "Hakuna kuleta madhara wala kujidhuru" na kauli ya Mtume S.A.W إنّما الْأَعْمَالُ بِالنِّيَّاتِ "Hakika matendo yanaendana na nia" na kauli ya Mtume S.A.W الدِّينُ النَّصِيحَةُ "Dini ni kupeana nasaha" na kauli yake S.A.W:

مَا نَهَيْتُكُمْ عَنْهُ فَاجْتَنِبُوهُ، وَمَا أَمَرْتُكُمْ بِهِ فَأْتُوا مِنْهُ مَا اسْتَطَعْتُمْ.

"Nilichokukatazeni basi jitengeni nacho, na nilichowaamrisha basi kileteni kama muwezavyo"(1).

Hakuna anayejenga hoja katika nafasi ya Sunna Takatifu za Mtume na umuhimu wake pamoja na ukubwa wa nafasi yake isipokuwa mpingaji au mbishi, Wanachuoni wamekubaliana kuwa Sunna Takatifu za Mtume S.A.W ni chanzo cha pili cha Sharia, kwa sababu hiyo kulikuwa na usimamizi mzuri zaidi kwa upande wa kuhifadhi upokezi uandishi ushereheshaji unyambuaji wa hukumu

(1) Kitabu cha Jaami Al-uluum cha Ibn Rajabu Al-Hambaly, ukurasa wa 62.

tofauti na msimamo wa baadhi ya wenye ufahamu mdogo wa uwazi wa maandiko ya Hadithi pasi ya kufahamu makusudio yake kumewapelekea kuganda na kujifunga kwenye kadhia nyingi, jambo linalozalisha mazungumzo kuhusu ufahamu wa makusudio ya Sunna za Mtume ni jambo muhimu sana na linahitajika mno ili kuvunja mzunguko huu wa mgando na kujifungia na kuzuilika kifikra.

Hakuna shaka kuwa Sunna zimekuja zikisherehesha kubainisha na kutimiliza Quran Tukufu, kwani Anasema Mola Mtukufu:

﴿وَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ وَلَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ﴾.

﴿**Nasi tumekuteremshia wewe Ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyo teremshwa kwao, wapate kufikiri**﴾[1]. Na anasema tena Mola Mtukufu:

(1) An-Nahli: 44

﴿وَأَنزَلَ الله عَلَيْكَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَعَلَّمَكَ مَا لَمْ تَكُن تَعْلَمُ وَكَانَ فَضْلُ الله عَلَيْكَ عَظِيمًا﴾.

**﴿Na Mwenyezi Mungu amekuteremshia Kitabu na hekima na amekufundisha uliyokuwa huyajui. Na fadhila za Mwenyezi Mungu zilizo juu yako ni kubwa﴾**[1]. Na anasema tena:

﴿هُوَ الَّذِي بَعَثَ فِي الْأُمِّيِّينَ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَإِن كَانُوا مِن قَبْلُ لَفِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ﴾.

**﴿Yeye ndiye aliye mpeleka Mtume kwenye watu wasiojua kusoma, awasomee Aya zake na awatakase, na awafunze Kitabu na hekima, ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu mkubwa﴾**[2]. Na Anasema tena Mola Mtukufu:

﴿وَاذْكُرُوا نِعْمَتَ الله عَلَيْكُمْ وَمَا أَنزَلَ عَلَيْكُم مِّنَ الْكِتَابِ وَالْحِكْمَةِ يَعِظُكُم بِهِ وَاتَّقُوا الله وَاعْلَمُوا أَنَّ الله بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ﴾.

**﴿Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu, na aliyo kuteremshieni katika Kitabu**

(1) An-Nisaa: 113.
(2) Al-Jumaa: 2

**na hekima anacho kuonyeni kwacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu﴾**[1]. Na akasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**﴿وَاذْكُرْنَ مَا يُتْلَى فِي بُيُوتِكُنَّ مِنْ آيَاتِ الله وَالْحِكْمَةِ إِنَّ الله كَانَ لَطِيفًا خَبِيرًا﴾.**

**﴿Na kumbukeni yasomwayo majumbani mwenu katika Aya za Mwenyezi Mungu na hekima. Kwa hakika Mwenyezi Munguni Mjuzi wa mambo ya siri, na Mwenye habari﴾**[2].

Hassan Al-baswary [3] na Imamu Shaafy [4] R.A

---

(1) Al-Baqarah: 231

(2) Al-Ahzaab: 34.

(3) Hassan Ibn Yasar Al-Baswary katika Taabii, alikuwa Imamu wa watu wa Baswarah, na msomi wa Umma katika zama zake, alifariki mwaka 110 H.

(4) Ni Abdillah Muhammad Ibn Idrisa Shaafy Mkuraishy, ni Imamu wa tatu katika Maimamu wanne wa watu wa Sunna na Jamaa, ndio mwenye madhehebu ya Shaafy na muanzilishi wa elimu ya asili ya Fiqhi, alizaliwa huko Ghaza mwaka 150 H, miongoni mwa vitabu vyake muhimu: Kitabu Al-Ummu, na Ar-Risaalah, nacho ni kitabu cha kwanza kutungwa kwenye elimu ya asili ya Fiqhi, alifariki nchini Misri mwaka 204 H.

na wengine miongoni mwa watu wa elimu na wafasiri wengi kuwa, hekima hapa ni Sunna za Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W [1].

Wanachuoni wamezungumza kwa kina kuhusu umuhimu wa Hadithi, anasema Imamu Shaafy Mungu amrehemu: Mwenyezi Mungu Mtukufu amemuweka Mtume wake S.A.W katika dini yake ibada zake na Kitabu chake kwenye sehemu aliyoiweka wazi Mola Mtukufu kuwa amemfanya ni elimu kwa dini yake kutokana na ulazima aliouweka wa kumtii, na akaharamisha kumuasi, akabainisha ubora wake kwa kukutanisha kumuamini Mtume wake S.A.W pamoja na kumuamini Yeye Mola Mtukufu, Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بالله وَرَسُولِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا وَجَاهَدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ الله أُولَئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ﴾.

(1) Rejea katia hayo Tafasiri ya Twabary na Ibn Katheer na wengine kwenye Aya ya 129 ya Suratul-Baqarah.

**﴿Hakika Waumini ni wale walio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake tena wasitie shaka kabisa, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao. Hao ndio wa kweli﴾**(1). Akafanya ukamilifu wa kuanza kwa imani kunafuata kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, ikiwa mja atamuamini Mwenyezi Mungu bila ya kumuamini Mtume wake basi hatokuwa kabisa na jina la ukamilifu wa imani mpaka pale atakapo muamini pamoja na Mtume S.A.W (2).

Na anasema R.A: Sijawahi sikia mtu yeyote watu wakimnasibisha au yeye mwenyewe akijinasibisha na elimu iliyo kinyume na alivyofatadhisha Mwenyezi Mungu Mtukufu kufuata amri ya Mtume S.A.W na kufuata hukumu zake kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu hakufanya kwa yeyote

(1) Al-Hujraat: 15.

(2) Kitabu cha Risalah cha Imamu Shaafy, kimefanyiwa uhakiki na Sheikh Ahmad Shaakir,1/75 chapa ya Dar al-Kutub al-ilmiyah Beirut.

baada yake isipokuwa ni mfuasi wake, na kuwa hakuna kauli inayolazimisha kwa hali yeyote ile isipokuwa ni kwa Kitabu cha Mwenyezi Mungu au Sunna za Mtume wake S.A.W ama kauli zisizokuwa hizo basi ni zenye kufuata tu, na ulazima wa Mwenyezi Mungu aliouweka kwetu na kwa wale watakaokuja baada yetu na waliokuwepo kabla yetu katika kukubali habari kuhusu Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W ni mmoja(1).

Na anasema Ibn Hazmi (2) R.A: Ni sehemu gani ndani ya Quran imeelezea swala ya adhuhuri ina rakaa nne, na swala ya Magharibi ina rakaa tatu, na kurukuu kwa namna hii na kusujudu kwa namna hii, na namna ya kusoma ndani ya swala na kutoa salamu, pia kubainisha yanayopaswa kuepukwa

---

(1) Kitabu cha Ummu cha Imamu Shaafy, kitabu ujumuisho wa elimu 7/287 chapa ya Dar Al-Maarifa Beirut.

(2) Naye ni Abu Muhammad Ally Ibn Ahmad Ibn Said Ibn Hazimi Al-Andulus Al-Qurtwuby, miongoni mwa Wanachuoni wabubwa wa Andulus, vitabu vyake muhimu ni pamoja na kitabu cha Al-Mahally Twuuq Al-hamama na vyengine, alifariki mwaka 456 H/ 1064.

kwenye ibada ya funga, na kuelezea namna ya utekelezaji wa ibada ya zaka ya dhahabu na fedha mbuzi ngamia na ng'ombe, kiwango kinachochukuliwa kwenye zaka, kiwango cha zaka inayochukuliwa, na ufafanuzi wa matendo ya ibada ya hija na muda wa kusimama milima ya Arafah, na sifa ya swala kuswaliwa eneo la Muzdalifa, kurusha vijiwe, namna ya kuhirimia, na yanayopaswa kuepukwa kwenye hija, namna ya kumkata mwizi mkono, unyonyeshaji ulio haramu, na vyakula vilivyoharamishwa, namna ya kuchinja, hukumu za makosa ya jinai, namna ya kukubalika talaka, hukumu za kuuza, ufafanuzi wa riba, mambo ya utoaji sadaka na mambo mengine ya aina za Fiqhi? Bali kilichomo ndani ya Quran ni amri za jumla lau tutaachwa na amri hizo tusingefahamu ni namna gani tunazifanyia kazi, lakini marejeo ya yote hayo ni kunukuu kutoka kwa Mtume S.A.W[1].

(1) Kitabu cha Ihkaam fii usuuli al-ahkaam cha Ibn Hazmi Adhahiry 2/79 Dar Al-Aafaq Al-Jadida Beirut.

Na anasema Shaukany[1] R.A: Jua kuwa wamekubaliana Wanachuoni kuwa Sunna Takatifu zinajitegemea katika kuweka hukumu, na zenyewe ni kama Quran katika kuhalalisha kilichohalali na kuharamisha kilichoharamu, na imethibiti kuwa Mtume S.A.W amesema: “Fahamu mimi nimepewa Quran pamoja na mfano wake” [2]. Kwa maana nimepewa Quran na nimepewa mfano wake miongoni mwa Sunna ambazo hazijatamkwa na Quran, na katika hayo ni kama vile kuharamishwa kwa nyama ya punda anayefugwa, uharamu wa nyama ya kila mnyama mwenye kuuwa kwa meno miongoni mwa wanyama wakali na wenye kuuwa kwa kucha miongoni mwa ndege, na visivyokuwa hivyo miongoni mwa mambo mengi[3].

(1) Muhammad Ibn Ally Ibn Muhammad Ibn Abdullah Shawkany, ni Mwanachuoni mwenye kujitahidi katika Wanachuoni wakubwa wa Yemen, miongoni mwa vitabu vyake muhimu ni pamoja na: Naili Al-Awtwar, Fathul Qadiir, alifariki huko Swanaa mwaka 1759H – 1834.

(2) Ni kitabu cha Ahmad 28/410. Hadithi nambari 17174.

(3) Kitabu cha Irshaad Al-Fuhul cha elimu ya asili cha Shaukany 1/96 chapa ya Dar Al-Kitabu Al-Araby.

Na anasema: Kwa ujumla ni kuwa kuthibiti kwa umuhimu wa Sunna Takatifu na kujitegemea kwake katika kuweka hukumu ni muhimu kidini, wala hapingi kwenye hilo isipokuwa kwa yule asiye na nafasi katika dini ya Uislamu(1).

Na anasema Imamu Al-Aluusy (2) R.A: أَطِيعُواْ اللهَ ﴿**Mtiini Mwenyezi Mungu**﴾ kwa maana wajibikeni kumtii katika yale aliyokuamrisheni na kukukatazeni. Na neno la Mwenyezi Mungu: وَأَطِيعُواْ الرَّسُولَ ﴿**Na mtiini Mtume**﴾ aliyeletwa ili kufikisha hukumu zake kwenu katika kila alichokuamrisheni na pia kukukatazeni, kurudia kitenzi - pamoja na kuwa kumtii Mtume kunafungamana na kumtii Mwenyezi Mungu Mtukufu – ni kuinua nafasi

(1) Kitabu cha Irshaad Al-Fuhuuli 1/96.
(2) Ni Mahmud Shihab deen al-Aluusy, akinasibishwa na mji wa Alus nao ni kisiwa katikati mwa mto wa Furat ndani ya mkoa wa Al-Ambar, mfasiri mtu wa Hadithi mwanachuoni wa Fiqhi mwanafasihi na mshairi, alifanya kazi ya kufutu maswala ya dini nchini kwake mwaka 1248H kisha akaachana na mambo ya elimu, miongoni mwa vitabu vyake muhimu: Tafasiri ya roho Al-Maany, alifariki mwaka 1270H – 1854.

yake S.A.W na kuondoa kabisa kudhaniwa kuwa hakuna wajibu wa kufuata isipokuwa yaliyomo ndani ya Quran tu, na kuonesha kuwa Mtume S.A.W anajitegemea kwenye utiifu ambapo haijathibiti kwa mwengine yeyote[1].

Na anasema Mwalimu Abdulwahaab Khalaf [2] R.A: Sunna ima iwe ni Sunna fafanuzi na yenye kufafanua yoliyokuja kwa maana jumla ndani ya Quran, au kuainisha yale yaliyokuja moja kwa

---

(1) Kitabu cha Roho Al-Maany katika tafasiri ya Quran Tukufu na kitabu cha Sabaa Minal-Mathaany cha Imamu Aluusy 5/65, chapa ya Dar Ihyaau Turaath Al-Araby Beirut.

(2) Ni mwana Hadithi na mwanafiqhi, ni mjumbe kweney baraza la lugha ya Kiarabu Cairo, alizaliwa mwaka 1888, ni mwenye vitabu vingi katika elimu ya asili ya Fiqhi, aliteuliwa kuwa kadhi katika mahakama ya Sharia mwaka 1920 kisha akahamishwa na kuwa mkurugenzi wa Misikiti ndani ya Wizara ya Waqfu mwaka 1924, akabakia kwenye nafasi hiyo mpaka alipoteuiwa kuwa mkaguzi wa mahakama za Kisharia kati kati ya mwaka 1931, alifanya kazi kama mwalimu kitengo cha masomo ya haki ndani ya Chuo Kikuu cha Cairo mwanzoni mwa mwaka 1939, akaendelea kuwa mwalimu wa Sharia ya Kiislamu mpaka akafikia umri wa kustaafu mwaka 1948, alifariki mwaka 1375H.

moja, au kubainisha umaalum katika yale yaliyokuja kwa wote, hivyo inakuwa tafasiri hii au uainishaji huu au umaalum huu ambao umeletwa na Sunna ni ubainifu wa kusudio la yaliyokuja kwenye Quran, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu amempa Mtume wake haki ya kubainisha Aya za Quran kwa kauli yake Mola Mtukufu:

﴿وَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ﴾.

**﴿Nasi tumekuteremshia wewe Ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyo teremshwa kwao﴾**[1]. Kwa maelezo haya: Sunna zimefafanua ibada ya swala kutoa zaka kuhiji, kwa sababu Quran imeamrisha ibada ya swala kutoa zaka na kuhiji bila ya kufafanua idadi ya rakaa za swala, wala makadirio ya zaka, wala utekelezaji wa ibada za hija, na Sunna za vitendo na kauli ndio ambazo zimebainisha ujumla huu wa ibada, vilevile kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **وَأَحَلَّ اللهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا ﴿Lakini Mwenyezi Mungu ameihalalisha**

(1) An-Nahli: 44

**biashara na ameiharimisha riba**﴿[1]. Na Sunna ndio ambayo imebainisha usahihi wa kuuza na ubaya wake, aina za riba haramu. Mwenyezi Mungu ameharamisha mzoga, na Sunna ndizo ambazo zimeelezea kusudio lake ukiacha mzoga wa samaki baharini na yasiyokuwa hayo miongoni mwa Sunna ambazo zimeelezea kusudio la ujumla uliokuja kwenye hukumu za Quran Tukufu, hivyo Sunna zinazingatiwa ni ukamilisho wake na makutano yake[2].

Kwa msingi wa yote yaliyotangulia kuanzia Aya za Quran Tukufu Sunna za Mtume Muhammad S.A.W na kauli za Wanachuoni inatubainikia wazi makubaliano ya Wanachuoni juu ya ukubwa wa nafasi ya Sunna za Mtume S.A.W, na umuhimu wake zikiwa zinasherehesha na kufasiri pamoja na kubainisha na kutimiliza, hakuna anayejen-

(1) Al-Baqarah: 275.

(2) Kitabu cha elimu ya asili ya Fiqhi cha Abdulwahab Khalaf ukurasa wa 40 chapa ya kitaubo cha uchapishaji wa kiraia nchini Misri.

ga mjadala katika hayo isipokuwa ni mpingaji au mbishi, au mtu asiye na nafasi yeyote katika elimu, wala mtazamo wake hauzingatiwi wala kuangaliwa na Wasomi.

***

# UTAFITI WA TATU

## Mtume wa Utu na Ubinadamu.

## S.A.W

Mtume wetu Muhammad S.A.W ni Mjumbe wa ubinadamu na Mtume wake, ni sawa kwa upande wa ujumbe wake umekuja kuwa ni rehma kwa walimwengu wote, au kwa upande wa kuwa ni ujumbe wa watu wote, ambapo Anasema Mola Mtukufu: ﴿وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَّةً لِّلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا﴾ **Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri, na mwonyaji**[1]. Na Mtume S.A.W anasema:

**وَكَانَ النَّبِيُّ يُبْعَثُ إِلَى قَوْمِهِ خَاصَّةً وَبُعِثْتُ إِلَى النَّاسِ كَافَّةً ، وَأُعْطِيتُ الشَّفَاعَةَ.**

“Na kila Mtume alikuwa anapelekwa kwa watu wake maalum, mimi nimepelekwa kwa watu wote

(1) Sabai: 28.

na nimepewa nafasi ya uombezi" [1], au imekuwa hivyo kwa upande wa yanayokusanya ujumbe wake ikiwa ni huruma ubinadamu na ukaribu kwa mwanadamu ni kwakuwa kwake ni mwanadamu pasi ya kuangalia dini yake au rangi yake au utaifa wake au lugha yake, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

﴿وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ﴾.

﴿**Na hakika tumewatukuza wanadamu**﴾[2]. Au kwa upande wa kutanguliza kwake Mtume S.A.W pande za ubinadamu katika mashirikiano yake yote na matendo yake mengine.

Na unaonekana wazi upande wa kibinadamu katika maisha ya Mtume S.A.W katika mashirikiano yake na Maswahaba zake wake zake wajukuu

(1) Imekubaliwa kwenye: Sahihi Bukhary, kitabu cha kutayamamu, mlango huo wa kutayamamu nambari 139 Hadithi nambari 335, na sahihi Muslimu, kitabu cha mambo ya Misikiti, Hadithi nambari 1191.
(2) Al-Israa: 70.

zake na watu wote, kwani alikuwa ni mtu bora kwa familia yake, naye anaseme kuhusu Mama wa Waumini Bi Khadija R.A: "Aliniamini wakati ambapo watu walinipinga, akaamini ukweli wangu wakati ambapo watu wana nikadhibisha, akaniliwaza kwa mali zake wakati ambapo watu wakinizuia kwenye mali, na Mwenyezi Mungu Mtukufu akaniruzuku mtoto wake ambapo watu waliponizuilia watoto wao" [1], aliendelea kuwa msaidizi mkubwa wakati wote wa uhai wake

(1) Kitabu cha Imamu Ahmad 54/215. Hadithi nambari 25606, na kitabu cha Mustadraki mlango wa Imani, Hadithi nambari 40. Na akasema: Hadithi hii ni sahihi kwa masharti ya Masheikh wawili, na akaipitisha Imamu Dhahaby. Ndani ya sahihi Bukhary inapatikana kwenye kitabu cha sifa za Answar, mlango wa kuoa kwa Mtume Bibi Khadija. Hadithi nambari 3818, na tamko lake kutoka kwa Bibi Aisha R.A amesema: Sijawahi kufanya wivu kwa mke yeyote wa Mtume S.A.W kama nilivyofanya wivu kwa Bibi Khadija, sijamuona lakini Mtume S.A.W alikuwa akimtaja sana, kwani huenda alikuwa anachinja mnyama na kukatakata nyama yake na kuipeleka kwa marafiki wa Bibi Khadija, pindi nilipomwambia hivi hakuna mwanamke mwengine duniani ispokuwa Khadija anasema: "Hakika alikuwa na alikuwa, na nilipata naye mtoto".

mpaka kifo chake, na Mtume alikuwa akiwakirimu marafiki wa Bibi Khadija na wale waliokuwa wanakuja wakati za zama zake, siku moja alikuja bibi mtu mzima nyumbani kwa Mtume S.A.W na Mtume akamuuliza: "Ni nani wewe? Akajibu mimi ni Jathamah Al-Muzaniyah, akasema Mtume: Bali wewe ni Hassanah Al-Muzaniyah, vipi hali zenu? Na namna gani mumekuwa mbali na sisi?" akajibu bibi tunaendelea vizuri ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, alipoondoka Bibi Aisha akamwambia Mtume, unampokea bibi huyu kwa mapokezi haya? Mtume S.A.W akasema: Kwa kweli alikuwa anakuja kwetu wakati wa uhai wa Bibi Khadija, na Kwa kweli ulikuwa ni wakati bora sana wa Imani"[1].

---

(1) Hadithi inapatikana kwenye kitabu cha Mustadraku kwenye sahihi mbili eneo tulilotaja hapo mwanzo, Imamu Bukhary alifasiri sehemu ya matini kwenye moja ya milango sahihi, na hiyo ni katika kitabu cha mambo ya adabu, mlango wa zama bora za imani, hadithi nambari 6004, na tamko lake ni kutoka kwa Bibi Aisha R.A amesema: "Sijawahi kufanya wivu kwa mwanamke kama nilivyofanya wivu kwa Bibi Khadiaj….. Hadithi.

Na Mtume S.A.W alikuwa ni mwenye mapenzi sana kwa wajukuu zake pamoja na uangalizi kwao. Abibakri amesema: Nimemuona Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W kwenye memberi na Hassan Ibn Ally akiwa pembezoni mwake, naye Mtume akiwa anawaangalia watu na wakati mwengine akimuangalia mjukuu wake na anasema: "Mjukuu wangu huyu ni kiongozi huenda Mwenyezi Mungu akampa uwezo wa kusuluhisha kati ya makundi makubwa mawili ya Waislamu"(1), pindi Aqlaa Ibn Habis alipomuona Mtume S.A.W akiwabusu Hassan na Hussein akasema: Mimi nina watoto kumi na mmoja sijahi kumbusu yeyote kati yao, ndipo Mtume S.A.W akamuangalia kisha akasema: "Mtu asiye na huruma hatofanyiwa huruma" na katika mapokezi mengine "Je naweza kuingiza huruma kwenye moyo wako baada ya Mwenyezi Mungu kuiondoa" (2).

---

(1) Ni Hadithi ndani ya sahihi Bukhary kitabu cha usuluhishi malango wa kauli ya Mtume S.A.W kwa Hassan Ibn Ally R.A mjukuu wangu huyu ni kiongozi, Hadithi nambari 2704.

(2) Imekubaliwa kwenye kitabu cha: Sahihi Bukhary kitabu cha

Na alikuwa Mtume S.W.A ni mwingi wa huruma kwa watu na hasa kwa upande wa watoto wadogo na watu wanyonge, ambapo anasema Mtume S.A.W:

إِنِّي لَأَقُومُ فِي الصَّلاَةِ أُرِيدُ أَنْ أُطَوِّلَ فِيهَا ، فَأَسْمَعُ بُكَاءَ الصَّبِيِّ ، فَأَتَجَوَّزُ فِي صَلاَتِي كَرَاهِيَةَ أَنْ أَشُقَّ عَلَى أُمِّهِ.

"Mimi nikiwa kwenye swala nikataka kurefusha kisomo kisha nikasikia sauti ya mtoto analia basi ninaifupisha swala yangu kwani ninachohofia uzito kwa mama yake" (1), na ansema Mtume S.A.W:

---

Adabu mlango wa huruma kwa watoto pamoja na kuwabusu, ni Hadthi nambari 5998. Na kwenye sahihi Muslimu kitabu cha mambo bora mlango wa huruma yake Mtume S.A.W kwa watoto pamoja na kuwatukuza, ni Hadithi nambari 6169.

(1) Imekubalika kwenye: Sahihi Bukhary kitabu cha adhana, lango wa kufupisha swala wakati wa kulia mtoto mdogo. Hadithi nambari 7070. Na katika kitabu cha sahihi Muslimu, kitabu cha swala mlango wa kuwataka Maiamamu kufupisha ibada ya swala. Hadithi nambari 1083, na tamko lake amesema Anasi: "Mtume S.A.W alikuwa anasikia kilio cha mtoto mdogo akiwa na mama yake naye Mtume akiwa kwenye ibada ya swala, basi anasoma Sura nyepesi au Sura fupi"

فَمَنْ صَلَّى بِالنَّاسِ فَلْيُخَفِّفْ، فَإِنَّ فِيهِمُ الْمَرِيضَ وَالضَّعِيفَ وَذَا الْحَاجَةِ.

"Mwenye kuwaswalisha watu basi asirefushe swala kwani miongoni mwa anaowaswalisha wapo miongoni mwao wagonjwa na watu dhaifu pamoja na wenye mahitaji mbalimbali" (1).

Na huyu hapa Mtume S.A.W macho yake yakitiririka machozi wakati alipofariki mtoto wake Ibrahimu Amani ya Mungu iwe kwake, ndipo Abdilrahman Ibn Aufu Rehma za Mungu ziwe kwake aliposema: Na wewe ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema Mtume S.A.W: "Ewe Ibn Aufu yenyewe ni huruma" kisha akasema: "Hakika jicho linatoa machozi, moyo unahuzunika, wala hatuna la kusema isipokuwa yale yanayomridhia

(1) Imekubaliwa kwenye: Sahhi Al-Bukhary kitabu cha elimu, mlango wa kukasirika kwenye mawaidha na mafunzo pindi mtu anapoona yanaomchukiza. Hadithi nambari 90. Na katika sahihi Muslimu, kitabu cha swala mlango wa kuwataka Maimamu kuwepesisha ibada ya swala. Hadithi nambari 1074.

Mola wetu, kwa hakika kuondoka kwako ewe Ibrahimu kunahuzunisha" [1].

Siku moja Mtume S.W.A alisujudu na alirefusha kusujudu kwake baada ya kumaliza ibada ya swala watu wakamuuliza Mtume: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, umesujudu mbele yetu kwenye swala yako hii na umerefusha sijida, tukadhani kuwa kuna jambo limetokea, au umeshushiwa ufunuo, akasema Mtume S.A.W: "Yote hayo hayapo, bali mjukuu wangu alinipanda kwa juu hivyo sikupenda kumuharakisha mpaka amalize mchezo wake" [2].

---

(1) Imekubalika: Kwenye sahihi Bukhary, kitabu cha jeneza mlango wa kauli ya Mtume S.A.W "Hakika kwa ajili yako ni wenye kuhuzunika" Hadithi nambari 1303. Na katika sahihi Muslimu kitabu cha mambo bora, mlango wa huruma yake S.A.W kwa watoto wadogo na upole wake kwao. Hadithi nambari 6167, na tamko lake: "Jicho linatoa machozi moyo unahuzunika wala hatusema isipokuwa yale yanayomridhisha Mola wetu, naapa kwa Mwenyezi Mungu ewe Ibrahimu kwako sisi ni wenye huzuni kubwa".

(2) Sunani An-Nisaaiy kitabu cha utekelezaji malango wa je inafaa sijda kuwa ndefu zaidi. Hadithi nambari 1141.

Kutoka kwa Abi Qatadah Al-Answary R.A amesema kuwa "Mtume S.A.W alikuwa anaswali akiwa amembeba mjukuu wake wa kike mtoto wa Zainabu binti wa Mtume S.A.W, pindi anaposujudu anamteremsha na anaposimama anambeba" [1]. Na pindi Mtume S.A.W alipokuwa anatoa hotuba akiwa kwenye membari akawaona Hassan na Hussein wanadondoka Mtume akateremka kwenye membari na kuwashika pamoja na kuwabusu, kutoka kwa Abdillah Ibn Buraidah, amesema: Nimemsikia Abi Buraidah anasema: Mtume alikuwa anatuhutubia punde akaja Hassan na Hussein wakiwa wamevaa kanzu nyekundu wanatembea wakiwa wamejikwaa, ndipo Mtume S.A.W akateremka kwenye membari akawabeba na kuwaweka mbele yake, kisha akasema: Amesema kweli Mwenyezi Mungu:

(1) Imekubaliwa: Kwenye sahihi Bukhary kitabu cha swala mlango wa pindi alipombeba mjukuu wake mdogo shingoni kwake akiwa kwenye swala. Hadithi nambari 516. Na katika sahihi Muslimu kitabu cha mambo ya Misikiti, mlango wa kufaa kubeba mtoto mdogo kwenye swala. Hadithi nambari 1240.

﴿إِنَّمَا أَمْوَالُكُمْ وَأَوْلادُكُمْ فِتْنَةٌ﴾ **Hakika mali zenu na watoto wenu ni fitina**﴾ nimewaangalia watoto hawa wawili wakiwa wanatembea na wakajikwaa sikuweza kusubiri mwisho nikakatiza mazungumzo yangu na kuwabeba [(1)].

Na alikuwa Mtume S.A.W anasema kuhusu Abibakri Swiddiq radhi za Mwenyezi Mungu ziwe kwake: "Hakika mtu muaminifu zaidi kwangu kwa ukaribu wake na mali zake ni Abubakri" [(2)], katika mapokezi mengine Mtume S.A.W alisema:

**«إِنَّ الله بَعَثَنِي إِلَيكُمْ فَقُلْتُمْ: كَذبْتَ ، وَقَالَ أَبُو بَكْرٍ: صَدَقَ ، وَوَاسَانِي بِنَفْسِهِ وَمَالِهِ ، فَهَلْ أَنْتُمْ تَارِكُو لِي صَاحِبِي.**

(1) Kitabu cha Sunani Abi Daud, kitabu cha swala mlango wa Imamu anakatisha hotuba kutokana na jambo lililotokea. Hadithi nambari 1109, na sunani ya Imamu Tirmidhy kitabu cha sifa, mlango wa sifa za Hassan na Hussein amani ya Mungu iwe kwao. Hadithi nambari 3774.

(2) Sahihi ya Imamu Bukhary, kitabu cha swala, mlango wa kupita Msikitini. Hadithi nambari 466. Na sunani ya Imamu Tirmidhy kitabu cha sifa mlango wa sifa za Abibakri Swaddiq Radhi za Mola ziwe kwake. Hadithi nambari 3660.

“Hakika Mwenyezi Mungu amenileta kwenu na mukasema: Unasema uwongo, Abubakri akasema umesema kweli, na akaniliwaza yeye mwenyewe na mali zake, basi niahieni rafiki yangu” (1), na alikuwa anasema kuhusu Sulaiman Al-Farisy: سَلْمَانُ مِنَّا أَهْلَ الْبَيْتِ “Sulaiman ni katika sisi watu wa nyumbani”(2), pindi aliporudi Jaafar Ibn Abitwal kutoka kwenye ufunguzi wa Khaibar, Mtume S.A.W alimbusu kwenye macho yake, na akasema S.A.W:

مَا أَدْرِي بِأَيِّهِمَا أَنَا أَفْرَحُ ، بِفَتْحِ خَيْبَرَ أَمْ بِقُدُومِ جَعْفَرٍ .

“Sifahamu kitu gani kati ya hivi viwili vinanipa furaha, ufunguzi wa Khaibar au kurudi kwa Jaafar” (3).

---

(1) Sahihi Bukhary kitabu cha sifa mlango wa kauli ya Mtume SAW aliyosema lau ningekuwa na rafiki wa karibu. Hadithi nambari 3661.

(2) Kitabu cha Muujamu Al-kabiir cha Twabrany 6/212. Hadithi nambari 6040, kitabu cha Mustadraki katika sahihi mbili, kitabu cha kuwafahamu Maswahaba Radhi za Mola ziwe kwao, kutajwa kwa Sulaimani Al-Faarisy R.A Hadithi nambari 6539.

(3) Kitabu cha Al-Mustadraki mlango wa kuhama kwa mara ya kwanza kuelekea Habasha. Hadithi nambari 4249.

Mtume S.A.W ametufundisha wema wa kibinadamu na hisia njema ndani ya wakati mmoja akasema: لاَ تَحْقِرَنَّ مِنَ الْمَعْرُوفِ شَيْئًا وَلَوْ أَنْ تَلْقَى أَخَاكَ بِوَجْهٍ طَلْقٍ "Usidharau sehemu ndogo ya wema hata kama kukutana na ndugu yako kwa sura ya bashasha" (1), na akasema tena Mtume S.A.W: لاَ تَحْقِرَنَّ جَارَةٌ لِجَارَتِهَا ، وَلَوْ فِرْسِنَ شَاةٍ "Jirani asimdharau jirani yake hata kwa kumpa kipande kidogo cha nyama ya mbuzi" (2), ni sawa sawa kwa upande wa kinachotolewa haipaswi kuhisi aibu kwa uchache au udogo wa unachokimiliki na ukakizuia kukitoa, kwani huenda dirham moja ikazidi dirham elfu moja, anasema Mtume S.A.W:

**مَنْ تَصَدَّقَ بِعَدْلِ تَمْرَةٍ مِنْ كَسْبٍ طَيِّبٍ - وَلاَ يَقْبَلُ الله إِلاَّ الطَّيِّبَ - وَإِنَّ الله يَتَقَبَّلُهَا بِيَمِينِهِ ، ثُمَّ يُرَبِّيهَا لِصَاحِبِهِ كَمَا يُرَبِّي أَحَدُكُمْ فَلُوَّهُ حَتَّى تَكُونَ مِثْلَ الْجَبَلِ.**

---

(1) Sahihi Muslimu kitabu cha wema undugu na adabu, mlango wa sunna kuleta bashasha unapokutana na ndugu yako. Hadithi nambari 6857.

(2) Imekubaliwa: Sahihi Bukhary kitabu cha utoaji zawadi. Hadithi nambari 2566. Sahihi Muslimu kitabu cha zaka mlango wa kuhimiza utoaji sadaka hata kama ni kidogo wala asizuie kidogo kwa kukidharau kwake. Hadithi nambari 2426.

“Mwenye kutoa sadaka kiasi cha tunda ya tende aliyoipata kwa njia halali – na wala hakikubaliki kwa Mwenyezi Mungu isipokuwa kilicho halali – na Mwenyezi Mungu akipokea kwa ridhaa yake, kisha anakikuza kwa ajili ya mwenye kukitoa kama vile mmoja wenu anavyokuza ndama wake mpaka sadaka inakuwa kama vile mfano wa mlima” (1), au ikiwa hilo kwa upande wa mwenye kuchukuwa ambapo haipaswi kukerwa mwenye kutoa pamoja na anachokitoa kidogo, bali tunapaswa kushukuru alichokitoa hata kama ni kidogo, ambapo anasema Mtume S.A.W: مَنْ لَمْ يَشْكُرِ النَّاسَ لَمْ يَشْكُرِ الله “Mtu asiyeshukuru watu hatomshukuru Mwenyezi Mungu” (2), hayo ni katika aliyoyasisitiza Abdillah Ibn Abbas R.A katika

(1) Imekubaliwa: Sahihi Bukhary kitabu cha mambo ya zaka mlango wa kutoa sadaka inayotokana na kipato halali. Hadithi nambari 1410. Na sahihi Muslimu kitabu cha zaka mlango wa kukubalika kwa sadaka iliyopatikana kwa njia halali na kuikuza. Hadithi nambari 2389.

(2) Sunani ya Imamu Tirmidhy kitabu cha wema na kuunga undugu, mlango wa yaliyokuja katika kushukuru kwa yule aliyekufanyia wema. Hadithi nambari 2082.

mazungumzo yake kuhusu wasia kumi ndani ya Suratul-Al-An'aam.

Hivyo basi, swala la kukuza maadili ya kibinadamu si jambo tu la kiutu, bali lenyewe ni Imani Sharia na dini tunayoifuata kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, badala ya umma kuvutana na kuuwana wao kwa wao pamoja na kufanya kazi ya kumalizana na kutiana udhaifu au kugawanyika wanapaswa kusaidiana na kushirikiana wote kwa maslahi ya wanadamu wote, ambapo Mola Mtukufu Anasema:

﴿يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَى وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا﴾.

﴿**Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane**﴾[1]. Lau wanadamu wote wangetoa ili kutibia tatizo la njaa umasikini maradhi pamoja

(1) Al-Hujraat: 13.

na maendeleo, sawa na kiwango kinachotolewa kwa ajili ya kuendeshea mapigano vita na uharibifu basi kwa hakika hali za watu zingebadilika na kuwa bora kwenye dini yao na dunia yao.

***

# UTAFITI WA NNE

## Kumpenda Mtume wa Mwenyezi Mungu Ni sehemu isiyogawanyika katika Imani.

Kumpenda Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W ni sehemu isiyogawanyika katika Imani, kwani anasema Abdillah Ibn Hishaam R.A:

**كُنَّا مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَهُوَ آخِذٌ بِيَدِ عُمَرَ بْنِ الْخَطَّابِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فَقَالَ: وَاللَّهِ لَأَنْتَ يَا رَسُولَ اللَّهِ أَحَبُّ إِلَيَّ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ إِلَّا نَفْسِي، فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ : وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ ، لَا يُؤْمِنُ أَحَدُكُمْ حَتَّى أَكُونَ أَحَبَّ إِلَيْهِ مِنْ نَفْسِهِ ، قَالَ عُمَرُ : فَأَنْتَ الْآنَ وَاللَّهِ أَحَبُّ إِلَيَّ مِنْ نَفْسِي، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ : الْآنَ يَا عُمَرُ.**

"Tulikuwa pamoja na Mtume S.A.W akiwa amemshika mkono Omar Ibn Khattab na akasema Omar: Naapa kwa Mwenyezi Mungu wewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ninakupenda zaidi

kuliko kitu chochote isipokuwa nafsi yangu, akasema Mtume S.A.W: Ninaapa kwa yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake, hatokuwa na imani mmoja wenu mpaka mimi niwe mwenye kupendwa zaidi kwake kuliko nafsi yake, akasema Omar: Hivi sasa naapa wewe ninakupenda zaidi kuliko nafsi yangu, kisha Mtume S.A.W akasema hivi sasa ewe Omar" (1), kwa maana hivi sasa imani yako imekamilika na kutimia.

**Na Mtume anasema tena:**

**"ثَلاثٌ مَنْ كُنَّ فِيهِ وَجَدَ حَلاوَةَ الإِيمانِ، أَنْ يَكُونَ اللهُ وَرَسُولُهُ أَحَبَّ إِلَيْهِ مِمّا سِواهُما، وَأَنْ يُحِبَّ الْمَرْءَ لا يُحِبُّهُ إِلاّ للهِ، وَأَنْ يَكْرَهَ أَنْ يَعُودَ في الْكُفْرِ كَما يَكْرَهُ أَنْ يُقْذَفَ في النَّارِ".**

"Mambo matatu mwenye kuwa ndani ya mambo hayo atapata uzuri na utamu wa Imani: Mwenyezi Mungu na Mtume awe ni mwenye ku-

---

(1) Sahihi Bukhary kitabu cha Imani na nadhiri, mlango wa namna gani kilikuwa kiapo cha Mtume S.A.W. hadithi nambari 6632.

wapenda zaidi: Ampende mtu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu: Achukie kurudi kwenye ukafiri kama anavyochukia kutupiwa motoni" (1), kuna mtu mmoja alikuja kwa Mtume S.A.W akasema: Kiyama kitakuja wakati gani? Mtume S.AW akasema: "Kwa kitu gani imejiandaa nacho kwa ajili ya hiyo siku?" Yule mtu akasema: Hakuna chochote isipokuwa mimi ninampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Mtume S.A.W akasema: "Basi wewe upo pamoja na unayempenda" (2).

Na kuna maneno yanayonasibishwa na Imamu Shaafy R.A kuwa amesema (3):

---

(1) Imekubalika: Sahihi ya Imamu Bukhary kitabu cha mambo ya Imani mlango wa raha ya Imani. Hadithi nambari 16. Sahihi Muslimu kitabu cha Imani mlango wa maelezo ya mambo atakayesifika nayo atapata raha ya Imani. Hadithi nambari 174.

(2) Imekubalika kwenye: Sahihi Bukhary kitabu cha ubora wa Maswahaba, mlango wa sifa za Omar Ibn Khattabu Abi Hafswin Al-Qurashy Al-Adawiy R.A. Hadithi nambari 3688. Na sahihi Muslimu kitabu cha wema kuunga undugu na adabu, mlango wa mtu pamoja na anayempenda. Hadithi nambari 6878.

(3) Wamemnasibisha Hafidhi Al-Manawy kwa Imamu Shaafy,

“Nawapenda waja wema na mimi si katika hao, huenda nikapata uombezi kutoka kwao. Ninamchukia ambaye biashara yake ni maasi, hata kama tutakuwa ni sawa sawa katika bidhaa”.

Ikiwa hivi ni kupenda waja wema, basi inakuwaje kwenu kwenye kumpenda mbora wa Mitume na mbora wa viumbe vyote vya Mwenyezi Mungu?

Kisha ni namna gani tusimpende Mtume S.A.W na kuyayuka kwenye upendo wake, naye ndiye ambaye Mwenyezi Mungu kupitia Mtume ametutoa katika kiza na kutuleta kwenye mwangaza, na akatuongoza kwenye njia ya Mwenyezi Mungu iliyonyooka, naye ndiye ambaye Mwenyezi Mungu ameinua utajo wake na kufunua kifua chake na

---

kitabu cha Faidhi al-kadiir sherehe ya Al-Jaami Swagiir cha Abdulrauuf Al-Manawy chapa ya Maktaba Tujaariyat Al-Kubraa 3/348. Na akasema Abu Naeem: Ametuambia Abu Al-Hassan Muhammad Ibn Muhammad Ibn Ubaidillah, amesema Aba Umayyah Al-Aswed: Nimemsikia Abdillah Ibn Al-Mubarak…. akamnasibisha kwa Abdillah Ibn Mubaraka.

kutakasa tabia zake na akamfanya muombezi bora na mbora wa kuomba, naye ndiye ambaye Mwenyezi Mungu humshushia rehma na kutuamrisha sisi kudumu kwenye kumtakia rehma na amani, pale Mola Mtukufu Aliposema:

﴿إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَاأَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا﴾.

﴿**Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Mtume. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu**﴾[1]. Na Anasema tena Mola Mtukufu kupitia ulimi wa Mtume wake S.A.W:

﴿قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ﴾.

﴿**Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu.**

(1) Al-Ahzaab: 56.

**Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu﴾**(1). Na Mwenyezi Mungu Mtukufu anaendelea kusema:

﴿وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللَّهَ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ لَوَجَدُوا اللَّهَ تَوَّابًا رَحِيمًا.

**﴿Na lau pale walipo jidhulumu nafsi zao wangeli kujia, wakamuomba Mwenyezi Mungu msamaha, na Mtume akawaombea msamaha, hapana shaka wangeli mkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu﴾**(2).

**Na Mtume S.A.W anasema:**

إِذَا سَمِعْتُمُ الْمُؤَذِّنَ ، فَقُولُوا مِثْلَ مَا يَقُولُ ، ثُمَّ صَلُّوا عَلَيَّ، فَإِنَّهُ مَنْ صَلَّى عَلَيَّ صَلَاةً صَلَّى الله عَلَيْهِ بِهَا عَشْرًا، ثُمَّ سَلُوا اللهَ لِيَ الْوَسِيلَةَ ، فَإِنَّهَا مَنْزِلَةٌ فِي الْجَنَّةِ ، لَا تَنْبَغِي إِلَّا لِعَبْدٍ مِنْ عِبَادِ اللهِ ،

(1) Aal-Imraan:31.
(2) An-Nisaai: 64.

وَأَرْجُو أَنْ أَكُونَ أَنَا هُوَ ، فَمَنْ سَأَلَ لِي الْوَسِيلَةَ حَلَّتْ لَهُ الشَّفَاعَةُ.

"Pindi mnaposikia muadhini, basi semeni mfano wa anavyosema, kisha nitakieni rehma kwani mwenye kunitakia rehma S.A.W ana thawabu kumi, kisha niombeeni kwa Mwenyezi Mungu Al-Wasiilah, kweni yenyewe ni sehemu ya juu Peponi, hapaswi kuwepo hiyo sehemu isipokuwa mja miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu, nategemea mimi kuwa ndio mwenyewe, hivyo mwenye kuniombea Al-Wasiilah amehalalikiwa maombezi" [1].

(1) Sahihi Muslimu, kitabu cha swala, mlango wa kusema mfano wa kauli ya muadhini kwa mwenye kumsikia, kisha kumtakia rehma Mtume SAW na kumuombea Wasiilah, hadithi nambari 384. Na katika Sunani ya Abi Daud: Kitabucha swala mlango wa anayosema wakati wa kumsikia muadhini. Hadithi nambari 523. Na sahihi Ibn Habban: Kitabu cha swala mlango wa adhana, imetajwa wajibu wa uombezi siku ya kiyama kwa mwenye kumuombea kwa Mwenyezi Mungu Mtume wake S.A.W Wasiilah wakati wa anaposikia adhana. Hadithi nambari 1690.

**Na anasema Hassan Ibn Thabiti** (1):

Mwenyezi Mungu ameliingiza jina la Mtume kwenye jina lake – pale anaposema muadhini mara tano Nashuhudia.

Na akapasua kwenye jina lake ili kumtukuza – basi kwenye Arshi ni Mahmoud na huyu ni Muhammad.

Tunasisitiza mambo mawili: jambo la Kwanza: Ni kuwa Wanachuoni na wachambuzi wa Hadithi baadhi yao wameangalia kauli ya Mtume S.A.W:

**لَا يُؤْمِنُ أَحَدُكُمْ حَتَّى أَكُونَ أَحَبَّ إِلَيْهِ مِنْ وَلَدِهِ وَوَالِدِهِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ.**

"Hawi na imani mmoja wenu mpaka mimi anipende zaidi kuliko watoto wake wazazi wake na watu wote" (2). Kuwa ni sharti katika masharti

(1) Kitabu cha Al-Bidaya wa An-Nihayah cha Ismail Ibn Omar Ibn Katheer Al-Qurashiy Abul-Fidaa 6/317.chapa ya Maktaba Al-Maarifu Beirut.

(2) Imekubalika na wapokezi wote: Imo kwenye sahihi Bukhary

ya ukamilifu wa Imani, kwa maana haikamiliki imani ya mtu isipokuwa kwa kuwa na upendo kwa Mtume, na wengine wakaangalia kuwa ni sharti miongoni mwa masharti ya kufaa kwa imani kwa maana haitofaa imani ya mtu isipokuwa kwa kumpenda Mtume S.A.W hayo ndio yenye kukubalika kwa upande wetu, ambapo ni namna gani tunasalimisha kufaa kwa imani kwa mtu asiyependwa?

Kauli nyengine: Ni kuwa upendo hauwezi kuwa kwa maneno tu, bali ni uzuri wa kuiga na uzuri wa kufuata pamoja na kujivisha tabia na maadili ya kipenzi S.A.W na kufuata uongofu wake, Imamu Shaafy anasema (1):

kitabu cha Imani mlango wa kumpenda Mtume S.A.W ni katika imani. Hadithi nambari 15. Katika sahihi Muslimu kitabu cha imani mlango wa wajibu wa kumpenda Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW. Hadithi nambari 92. Na sunani ya An-Nisaai kitabu cha Imani mlango wa alama za imani. Hadithi nambari 5029. Na sunanni Ibn Maja cha "Mukaddima" mlango katika Imani. Hadithi namba 67.

(1) Diwani ya Imamu Shaafy, kimefanyiwa uhakiki na Dr. Muhammad Abdulmuneem Khafajy ukurasa wa 91 chapa ya Maktaba ya Vitivyo vya Al-Azhar.

Unamuasi Mwenyezi Mungu na wewe unaonesha upendo wako wake – hili haliwezekani katika kipimo ni jambo la ajabu.

Lau ungekuwa upendo wako ni wa kweli basi ungemtii – kwa sababu mwenye kupenda kwa anayempenda ni mtiifu.

Mwenye kumpenda Mtume wa Mwenyezi Mungu hawezi kuwa mtu muwongo wala mwenye kughushi mambo, wala kuwa msaliti wala muovu wala mwenye kiburi wala mwingi wa kutukana bali anakuwa kama alivyosema Bibi Aisha R.A kuhusu Mtume S.A.W: **كَانَ خُلُقُهُ الْقُرْآنَ** "Tabia zake zilikuwa Quran"(1), na Mtume S.A.W alikuwa ni Quran inayotembea ardhini, au kama alivyosema Bibi Khadija R.A:

**.. كَلا وَاللَّهِ مَا يُخْزِيكَ اللَّهُ أَبَدًا ، إِنَّكَ لَتَصِلُ الرَّحِمَ ، وَتَحْمِلُ الْكَلَّ ، وَتَكْسِبُ الْمَعْدُومَ ، وَتَقْرِي الضَّيْفَ ، وَتُعِينُ عَلَى نَوَائِبِ الدهر ..**

(1) Kitabu cha Musnadi Ahmad 41/ 148. Hadithi nambari 24601.

"….Hapana Mwenyezi Mungu hatokupoteza, kwani wewe utaunganisha undugu, utawabeba watu wote, utampa aliyenyimwa, utamkirimu mgeni, na kumsaidia mwenye majukumu ya haki…." (1).

***

(1) Imepokelewa na Maimabu wote inapatikana kwenye: Sahihi Bukhary kitabu cha kuanza kwa ufunuo, mlango wa namna gani ulianza kushuka ufunuo kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW. Hadithi nambari 3. Na katika sahihi Mulimu kitabu cha Imani mlango wa kuanza kwa ufunuo kwa Mtume SAW. Hadithi nambari 422.

# UTAFITI WA TANO
## Kuwa na adabu na Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W

Kuwa na adabu na Mtume S.A.W kunapelekea mambo mengi miongoni mwa hayo mambo ni:

1- Kutotajwa jina lake S.A.W likiwa limeepukana na wasifu wa Utume au Ujumbe au kuswaliwa, ni sawa sawa wakati wa kutajwa kwake S.A.W au wakati wa kusikika jina lake S.A.W au kuandikwa jina lake S.A.W kwa idadi ya yeyote itakayo andikwa au kutajwa, hiyo ni katika alama maalum ya kumpenda Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W, na haya tunafundishwa na Quran Tukufu ambapo imekuja kauli ya Mungu ikiambatana na utukufu wa Ujumbe au Utume au sifa za ukarimu ubora na upole kama kauli ya Mwenyezi Mungu inayosema:

﴿يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ لاَ يَحْزُنكَ الَّذِينَ يُسَارِعُونَ فِي الْكُفْرِ﴾.

**﴿Ewe Mtume! Wasikuhuzunishe wa fanyao haraka kukufuru﴾**[1].

Na kauli yake Mola Mtukufu: **يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ حَسْبُكَ اللَّهُ وَمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ** **﴿Ewe Nabii! Mwenyezi Mungu anakutoshelezea wewe na Waumini walio kufuata﴾**[2]. Na kauli yake Mola Mtukufu: **يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ شَاهِدًا وَمُبَشِّرًا وَنَذِيرًا** **﴿Ewe Nabii! Hakika Sisi tumekutuma uwe shahidi na mbashiri na mwonyaji﴾**[3]. Na kauli ya Mola Mtukufu: **يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِنَّا أَحْلَلْنَا لَكَ أَزْوَاجَكَ اللَّاتِي آتَيْتَ أُجُورَهُنَّ** **﴿Ewe Nabii! Tumekuhalalishia wake zako ulio wapa mahari yao﴾**[4].

2- Kukithirisha kumtakia rehma Mtume S.A.W ambapo Mwenyezi Mungu Anasema: **إِنَّ اللَّهَ**

(1) Al-Maidah: 41
(2) Al-Anfaal:64
(3) Al-Ahzaab: 45,
(4) Al-Ahzaab: 50

**وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا﴾ ﴿Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Mtume. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu﴾**[1].

Anasema Ibn Katheer R.A: Makusudio ya Aya hii: Ni kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu amewapa habari waja wake juu ya nafasi ya mja wake na Mtume wake kwake kuwa anasifiwa na Malaika waliokaribu, na Malaika wanamtakia rehma, kisha Akaamrisha Mwenyezi Mungu Mtukufu watu wa ulimwengu wa chini kumtakia rehma na kumsalimu kwa salamu, ili sifa njema zikutane kwake kutoka kwa viumbe wote wa ulimwengu wa juu na chini [2].

Siku moja kuna mtu alikuja kwa Mtume S.A.W akasema: Nimesikia Mwenyezi Mungu Mtukufu

(1) Al-Ahzaab: 56.
(2) Tafsiir Ibn Katheer Suratul-Ahzaab 3/555 chapa ya Dar Al-Fikri. Beirut.

Anasema: ﴿إِنَّ اللهَّ وَمَلائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ....﴾ **Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Mtume** Aya, ni namna gani kukutakia rehma? Akasema Mtume S.A.W sema:

**اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّد وَعَلى آلِ مُحَمَّد ، كَمَا صَلَّيتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَميدٌ مَجيدٌ ، وَبَارك عَلَى مُحَمَّد وَعَلى آلِ مُحَمد ، كَمَا بَارَكتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ إنكَ حَمِيد مَجِيدٌ.**

"Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma kwa Muhammad pamoja na watu wa nyumbani kwa Muhammad, kama ulivyopeleka rehma kwa Ibrahimu kwani hakiki Yako ni mwenye sifa nzuri na utukufu, mshushie baraka Muhammad pamoja na watu wa nyumbani kwa Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahimu hakika Yako ni mwenye sifa njema na utukufu"[1].

---

(1) Sahihi Bukhary kitabu cha tafsiri ya Quran Suratul-Ahzaab, mlango wa kauli ya Mwenyezi Mungu: **﴿إِنَّ اللهَّ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا﴾**: Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Mtume. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa sal-

Na miongoni mwa kumfanyia adabu Mtume S.A.W ni kutofupisha muundo wa kumtakia rehma wakati wa kuandika kwa kuandika S.A.W badala ya kuandika Rehma na Amani ya Mwenyezi Mungu iwe kwake, ambapo inatupasa kuandika kikamilifu ili tusikose thawabu na fadhila nyingi[1].

3- Kutoshirikiana na Mtume kama tunavyo-shirikiana sisi kwa sisi, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: **لَّا تَجْعَلُوا دُعَاءَ الرَّسُولِ بَيْنَكُمْ كَدُعَاءِ بَعْضِكُم بَعْضًا﴿Msifanye wito wa Mtume kati yenu kama wito wa nyinyi kwa nyinyi﴾**[2]. Hali hiyo inapelekea pia kwenye kushirikiana na Sunna zake isiwe kama tuna-vyoshirikiana sisi kwa sisi, hilo limesisitizwa na Wanachuoni wakubwa ambapo anasema Imamu Abu Hanifa R.A: "Ikiwa nitasema kauli

amu﴾. Hadithi nambari 4519.

(1) Angalia: Utafiti wa sita: Katika fadhila za kumtakia rehma Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W ukurasa wa 71.

(2) An-Nuur: 63

inayopingana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu pamoja na Sunna za Mtume S.A.W basi iacheni kauli yangu" [1].

Na anasema Imamu Maliki R.A: "Hakuna yeyote baada ya Mtume S.A.W isipokuwa kauli yake inachukuliwa na kuachwa ila kauli ya Mtume S.A.W. na anasema: "Kwa hakika mimi ni mwanadamu ninafanya makosa na ninapatia, basi angalieni rai yangu kila kinachokubaliana na Kitabu pamoja na Sunna kichukueni, na kila kinachopingana na Kitabu pamoja na Sunna kiacheni"[2].

Na anasema Imamu Shaafy R.A: "Hakuna mtu yeyote isipokuwa atafuata mwenendo wa Mtume wa Mungu S.A.W basi nitakavyosema au kufikia asili katika asili mbalimbali ndani yake ikawa ni kinyume na aliyoyasema Mtume S.A.W basi kauli

(1) Kuamsha umuhimu wa watu wenye muono ni kitabu cha Mwanachuoni Al-Fulany ukurasa wa 93 chapa ya Dar Al-Kutubi Al-Aalamiayah, Beirut Lebanon.
(2) Kitabu cha Majmuui cha Imamu An-Nawawy 1/175 Dar Al-Kutubi Al-Aalamiyah Bairuti Lebanoni.

ni aliyoisema Mtume S.A.W na hiyo ndio kauli yangu" [1]. Na anasema pia: "Pindi munapokuta kwenye kitabu changu tofauti na Sunna ya Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W basi semeni yaliyo kwenye Sunna ya Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W na yaacheni niliyosema" [2].

Na anasema Imamu Ahmad Hambal R.A: "Usiniige mimi wala kumuiga Imamu Maliki wala Imamu Shaafy wala Imamu Al-Auzai wala Imamu Thawry bali chukua ambapo wamechukua" [3].

4- Kulazimika kwa viwango vya juu kabisa vya adabu na unyenyekezu ndani ya Msikiti wake S.A.W wala hakuna shaka kuwa utukufu wa kuwa jirani na Mtume wa Mungu S.A.W akiwa amefariki ni sawa sawa na ujirani wa uhai

(1) Kitabu cha Ilam Al-Muwaqiin cha Ibn Qayyim Al-Jauzy, kimefanyiwa uhakiki na: Muhammad Abdulsalaam Abrahimu 2/204 chapa ya 1, 1411H/ 1991, Dar Al-Kutubi Al-Ilmiya Beirut Lebanon.
(2) Kitabu cha Iilaam Al-Muwaqqin: 2/203.
(3) Chanzo kilichopita: 2/ 139.

wake, kwani Imamu Maliki siku moja alipata kumsikia mtu mmoja akinyanyua sauti yake ndani ya Msikiti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W akasema: Ewe unayefanya hivi, kuwa na adabu mbele ya hadhira ya Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwahi kuwasifu watu na akasema:

﴿إِنَّ الَّذِينَ يَغُضُّونَ أَصْوَاتَهُمْ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ أُولَئِكَ الَّذِينَ امْتَحَنَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ لِلتَّقْوَى لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ﴾.

**﴿Kwa hakika wanao teremsha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio Mwenyezi Mungu amezisafisha nyoyo zao kwa ucha-Mungu. Hao watakuwa na msamaha na malipo makubwa﴾**(1). Na akawalaumu watu kwa kusema:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَنْ تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تَشْعُرُونَ﴾.

---

(1) Al-Hujraat: 03.

﴿Enyi mlio amini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Mtume, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui﴾[1]. Na heshima ya Mtume wa Mwenyezi Mungu akiwa amefariki ni sawa sawa na alipokuwa hai.

***

(1) Al-Hujraat: 2.

## UTAFITI WA SITA
## Miongoni mwa ubora wa kumtakia rehma Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W

Kumtakia rehma na amani Mtume wa Mwenyezi Mungu kuna fadhila kubwa miongoni mwazo:

1- Kupata rehma ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuenea fadhila zake sawa na uwingi wa kumtakia rehma na amani Mtume wetu S.A.W: Ikiwa rehma kutoka kwa Mwenyezi Mungu ina maanisha huruma, basi Mtume S.A.W amesema:

**... من صلَّى عليَّ واحدةً صلَّى اللَّهُ عليهِ عشرًا..**

"Mwenye kunitakia rehma mara moja basi anathawabu kumi" [1].

(1) Imekubaliwa na Wanachuoni wa Hadithi: Ipo kwenye sahihi

**Na akasema pia:**

من ذُكِرْتُ عنــده فَلْيُصَــلِّ عليَّ ، ومـن صـلَّى عليّ مــرةً صَلّى اللهُ عليه عشرًا.

"Kwa mtu nitakayetajwa mbele yake basi anitakie rehma, na mwenye kunitakia rehma mara moja atapata thawabu kumi" (1).

2- Kuombewa msamaha na Malaika: Ambapo Mtume S.A.Wanasema:

ما مِن مُسلِمٍ يصلِّي عليَّ إلَّا صلَّت عليهِ الملائِكةُ ما صلَّى علَيَّ فليُقلَّ العَبدُ من ذلِكَ أو ليُكثِرْ.

"Muislamu yeyote akanitakia rehma isipokuwa na yeye huombewa msamaha na Malaika kwa ida-

---

Bukhary kitabu cha adhana mlango wa anayosema pindi anapomsikia muadhini. Hadithi nambari 611. Na katika sahihi Muslimu kitabu cha mambo ya swala mlango wa Sunna kusema kama anavyosema muadhini kwa yule anayemsiki kisha anamswalia Mtume SAW na kumuombea kwa Mwenyezi Mungu Al-Wasiilah. Hadithi nambari 875.

(1) Sunani An-Nisaay, mlango katika kumsalia Mtume S.A.W. hadithi nambari 9889.

di aliyonitakia mimi rehma, hivyo mtu anaweza kufanya kwa uchache au kwa wingi" (1).

3- Kuptata uombezi wa Mtume S.A.W, kutoka kwa Abdillah Ibn Amru Ibn Al-Aswi R.A alimsikia Mtume S.A.W anasema:

**إِذَا سَمِعْتُمْ الْمُؤَذِّنَ فَقُولُوا مِثْلَ مَا يَقُولُ ، ثُمَّ صَلُّوا عَلَيَّ ، فَإِنَّهُ مَنْ صَلَّى عَلَيَّ صَلاةً صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ بِهَا عَشْرًا ثُمَّ سَلُوا اللَّهَ لِي الْوَسِيلَةَ ، فَإِنَّهَا مَنْزِلَةٌ فِي الْجَنَّةِ لا تَنْبَغِي إِلا لِعَبْدٍ مِنْ عِبَادِ اللَّهِ ، وَأَرْجُو أَنْ أَكُونَ أَنَا هُوَ فَمَنْ سَأَلَ لِي الْوَسِيلَةَ حَلَّتْ لَهُ الشَّفَاعَةُ.**

"Pindi munapomsikia muadhini basi semeni mfano wa anavyosema, kisha nitakieni rehma, kwani mwenye kunitakia rehma mara moja ana malipo ya thawabu kumi, kisha muniombee kwa Mwenyezi Mungu Al-Wasiilah, kwani hiyo ni sehemu ya juu Peponi haipaswi isipokuwa kwa mja miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu, na nat-

(1) Sunani ya Ibn Maja, kitabu cha kusimamisha swala, mlango wa kumswalia Mtume SAW. Hadithi nambari 910.

egemea kuwa mimi ndio mwenyewe, hivyo mwenye kuniombea Wasiilah atakuwa amehalalikiwa uombezi" [1].

Na akasema Mtume S.A.W: أولى النَّاسِ بي يومَ القيامةِ أكثرُهم عليَّ صلاةً "Mtu bora kwangu siku ya kiyama ni yule mwenye kunitakia sana rehma" [2].

4- Kuinuliwa daraja na kufutiwa makosa na madhambi: Mtume S.A.W anasema:

مِن صلَّى عليَّ صلاةً واحدةً صلَّى اللَّهُ عليهِ عشرَ صلواتٍ ، وحُطَّت عنهُ عَشرُ خطيئاتٍ ، ورُفِعَت لَهُ عشرُ درجاتٍ.

"Mwenye kunitakia rehma mara moja anatakiwa rehma mara kumi, na hufutiwa makosa kumi, na kuinuliwa daraja kumi" [3].

---

(1) Sahihi Muslimu kitabu cha swala mlango wa kusema mfano wa anavyosema muadhini kwa mwenye kumsikia, kisha amswalie Mtume S.A.W na kumuombea Wasiilah. Hadithi nambari 384.

(2) Sunani ya Tirmidhiy milango ya witri, mlango uliokuja katika kuelezea ubora wa kumsaliwa Mtume S.A.W. hadithi nambari 484.

(3) Sunani An-Nisaai kitabu cha kusahamu mlango wa ubora wa kumtakia rehma Mtume S.A.W. hadithi nambari 1297.

Na kutoka kwa Abi Twalhah Al-Answary R.A amesema: Siku moja Mtume S.A.W alikuwa amejipamba vizuri zaidi na kuonekana usoni mwake kuna bishara, akaulizwa: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu leo umejipamba sana na kuonekana uso wako una bishara, akasema "Ndio, kwani amenijia mwenye kunijia kutoka kwa Mola wangu Mtukufu na akasema: Mwenye kukutakia rehma katika uma wako mara moja Mwenyezi Mungu humuandikia thawabu kumi na kufutiwa makosa kumi na kuinuliwa daraja kumi" (1).

5- Kutosheleza matatizo na kusamehewa dhambi: Kutoka kwa Abi Kaab R.A amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu mimi huwa nakutakia rehma kwa wingi je niwe nakutakia rehma mara ngapi? Akasema Mtume S.A.W unavyoweza, akasema robo siku, Mtume akas-

(1) Sunani Diramy kitabu cha utumwa mlango wa ubora wa kumswalia Mtume S.A.W. hadithi nambari 2773. Na Musnadi ya Ahmad 26/ 272. Hadithi nambari 16352.

ema unavyotaka ikiwa utazidisha basi ni bora kwako, akasema nusu siku, Mtume akasema tena unavyotaka ikiwa utazidisha ni bora zaidi kwako, nikasema: Theluthi mbili za siku, Mtume akasema kama unavyotaka ikiwa utazidisha ni bora kwako, nikasema je nikutakie rehma siku mzima? Akasema: kufanya hivyo Itakutosheleza na matatizo yako na kusamehewa dhambi zako" (1).

6- Heshima ya mwenye kumtakia rehma Mtume S.A.W kwa kufikishiwa Mtume S.A.W salamu zake, na Mutume S.A.W kujibu ambapo anasema:

**إنَّ للَّهِ ملائِكةً سيَّاحينَ في الأرضِ يبلِّغوني عن أمتيَ السَّلامَ.**

"Hakika Malaika wanatembea ardhini wananifikishia salamu za uma wangu" (2).

---

(1) Sunani Tirmidhy kitabu cha jumla ya milango ya sifa za kiyama. Hadithi nambari 2457.

(2) Sahihi Ibn Habban mlango wa maombi. Hadithi nambari 9114.

Na akasema tena: مَا مِنْ أَحَدٍ يُسَلِّمُ عَلَيَّ إِلاَّ رَدَّ اللهُ عَلَيَّ رُوحِي حَتَّى أَرُدَّ عَلَيْهِ السَّلاَمَ "Mtu yeyote akinisalimia isipokuwa Mwenyezi Mungu hurudisha roho yangu mpaka nimjibu salamu yake" (1).

Na Mtume S.A.W akasema tena:

**أَكْثِرُوا الصلاةَ عليَّ ، فإنَّ اللهَ وكَّلَ بي ملَكًا عند قبري، فإذا صلَّى عليَّ رجلٌ من أُمَّتِي قال لي ذلك المَلَكُ:يا محمدُ إنَّ فلانَ بنَ فلانٍ صلَّى عليك الساعةَ.**

"Zidisheni sana kunitakia rehma, kwani Mwenyezi Mungu ameniwakilishia Malaika kwenye kaburi langu, pindi mtu katika uma wangu anaponitakia rehma huyo Malaika huniambia: Ewe Muhammad fulani Ibn fulani amekutakia rehma kwa muda wa saa" (2).

Ubora na fadhila za kumtakia rehma mbora wa viumbe ambaye ni Mtume Muhammad S.A.W

(1) Musnadi Ahmad. Hadithi Abi Twalhah Zaidu Ibn Sahli Al-Answary kutoka kwa Mtume SAW 8/34. Hadithi nambari 16103.
(2) Musnadi Al-Bazar 2/266. Hadithi nambari 1241.

ni nyingi mno hazihesabiki, zipo zilizowazi idadi yake, na zengine zisizo onekana idadi, ambapo hafahamu namna ya kuwa kwake wala ujumla wa baraka zake isipokuwa kwa mwenye kuonja, na mwenye kuonja amefahamu, na mwenye kufahamu anakuwa na nguvu na mwenye nguvu amefika nafasi ya juu, inatosha kulazimika kupata utulivu wa nafsi na akili na utulivu wa moyo, na kufunguka kifua, kuonja ladha ya Imani, ambapo Mtume S.A.W anasema:

**ذَاقَ طَعْمَ الإِيمَانِ مَنْ رَضِىَ بِاللَّهِ رَبًّا وَبِالإِسْلاَمِ دِينًا وَبِمُحَمَّدٍ صلى الله عليه وسلم رَسُولاً.**

"Ameonja ladha ya Imani mwenye kuridhia kwa Mwenyezi Mungu kuwa Mola na Uislamu ni dini na Muhammad S.A.W kuwa ni Mtume" (1).

***

(1) Sahihi Muslim katika kitabu cha Imani mlango wa mwenye kuonja ladha ya Imani. Hadithi nambari 34,

# UTAFITI WA SABA
# Baadhi ya mashairi katika upendo na ubora wa Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W
# Mashairi ya Ahmad Shauqy katika kumsifu Mtume

*Uongofu umezaliwa ulimwengu ukiwa na mwangaza - Zama zikiwa na tabasamu na kusifu.*

*Malaika Jibril na Malaika wengine waliizunguka - Dini na dunia zilifurahia kuzaliwa kwake.*

*Mwenyzi Mungu amebashiria mbingu kwa kuzaliwa kwako na akazipamba - Na harufu nzuri imetoka na kusambaa ardhini.*

*Ulipozaliwa muonekano wako mzuri ulionekana - Na kujazwa uongofu na haya.*

*Na nuru ya utume ipo kwako na iking'ara Kutokana na kipenzi cha Mungu na uongofu wake umepewa alama zake.*

*Nabii Isa amemsifu akiwa mbinguni - Na bikira Maryamu alifurahi na kutikisika.*

*Siku iliyofuata asubuhi yake na mchana wake - Ilikuwa na nuru kwa sababu ya Muhammad.*

**Na anasema tena:**

*Unapofanya ukarimu unafika kiwango cha juu - Na kufanya yasiyofanywa na wenye ukarimu.*

*Na pindi unaposamehe ni mwenye uwezo na nguvu - Usiolinganishwa msamaha wako na wajinga.*

*Basi unaposamehe unakuwa kama baba au mama - Na wawili hawa ndio wapole zaidi duniani.*

*Na unapokasirika kwa hakika ni hasira - Katika haki huna chuki wala husuda.*

*Unaporidhia basi ni kwa kutafuta radhi zake Mungu - Na wengi wanaodai kuridhia*

*ni kwa majivuno na kujionesha.*

*Unapotoa hotuba basi mimbari hutetemeka - Unaeleza yaliyofichika na nyoyo hulia.*

*Unapohukumu hakuna shaka kana kwamba - Hukumu ya ugonvi imekuja kutoka mbinguni.*

*Unapoyalinda maji hawezi yapata - Hata watawala na wafalme wakiwa na kiu.*

*Unapompa mtu kazi basi wewe ni nyumba ya Mungu - Mfanyakazi hatoingiza humo madhara.*

*Unapomiliki nafsi unaitendea wema - Hata kama mkono wako umemiliki mbuzi*

*Unapojenga unakuwa mume mwema - Unapozaa watoto unakuwa baba bora.*

*Na unapofanya urafiki wema unaonekana - Kwa marafiki na watu wa karibu.*

*Na unamtendea mema mpumbavu na unamfanyia huruma - Hata kama wajinga watavunja heshima yako.*

*Nafsi zote zimepewa heshima yako - Na kila nafsi inategemea uombezi wako.*

*Ewe usiyejua kusoma wala kuandika una cheo kikubwa. Katika elimu mpaka Wanachuoni wanajifunza kwako.*

*Ama Hadithi zako kwenye akili ni chanzo cha Sharia - Na ni elimu na hekima iliyofunikwa na maji.*

*Katika tungo za mashairi ya Ahmed Shawky.*

*Nimesimama mlangoni mwa Kiongozi wa Nabii wote - Na anayeshika ufunguo wa mlango wa Mwenyezi Mungu anafaulu.*

*Na fadhila zote wema na shukrani - Ni kati ya mpokeaji na muwajibikaji.*

*Nimejifunga kamba kwa kumsifu kwake najifaharisha - Ndani ya siku ambayo hakuna kujifaharisha kwa ujamaa wala ukoo.*

*Muhammad mbora wa viumbe na mpole wake - Na ni bwana wa wanadamu wote na viumbe.*

*Na ni mwenye birika siku ambayo Mitume watamuuliza - Tutakunywa lini na Malaika Jibril ni mwenye kiu.*

**Anaendelea kusema:**

*Bahira alipomuona akasema tunamfahamu - Kutokana na tuliyoyajua miongoni mwa sifa na majina yake.*

*uliza pango la hiraa na Malaika jibril je wamejua - Siri iliyofichika kueleweka na kutoonekana.*

*Eneo la Makka lilifaharika mara ngapi - Kwa kwenda na kurudi kwake usiku na mchana kwenye pango hilo.*

*Na peke yake mtoto wa Abdillah akiwa kati ya maeneo hayo mawili - Akihangaika akiwa mbora wa wanadamu kwa nasaba na heshima.*

*Pana angaliwa na ufunuo kabla ya kushuka*

*kwake - Na anayebashiriwa na alama ya heri anaonekana.*

*Maswahaba walipomuomba maji kwa sababu ya kiu - Mikono yake ilitoa maji mazuri na safi.*

*Na mawingu yalivutiwa na mbora wa viumbe - Na yalikuwa kivuli cha kumlinda na yalikuwa kama rafiki yao.*

*Kwa mapenzi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu - Watumishi wa Mahekalu na Watawa pia wanampenda sana.*

*Hakika tabia za Mtume zimemfanya apendwe na vitu vyote - Na pia viumbe vyote vilivyo hai.*

*Na Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuamrisha soma - Hajawahi kumwambia kwa mdomo yeyote kabla yake.*

*Huko Mwenyezi Mungu aliruhusu na kujaa - Masikio ya watu wa Makka kwa nyimbo takatifu.*

*Usiulize namna Makuraishi walivyokataa ulinganiaji huo - Na namna gani walikanusha wakiwa bondeni na mlimani.*

*Na wakaulizana wamepatwa na jambo gani - Ambalo limewafanya wazee na vijana kulaumiana.*

*Enyi wajinga msiomjua Mtume na Sunna zake - Hivi mmekuwa wajinga juu ya nafasi ya mkweli wa ulimwengu.*

*Mumemsifu kuwa ni muaminifu wetu tangu udogo wake - Na je mnakuwa na shaka na kauli ya Muaminifu.*

*Ewe mfasaha wa wazungumzaji Kiarabu kinyume na wengine. - Mazungumzo yako ni matamu na ushahidi kwa wenye kufahamu ladha.*

*Kila kauli nzuri wewe ndio mzungumzaji wake - Huleta uhai na kufufua hima zilizokufa.*

**Anasema tena:**

*Watu wamemfurahia Mtume na kuzaliwa kwake - Mashariki na Magharibi ujio wa nuru katika giza.*

*Umeteka mfumo wa waovu miongoni mwa Waarabu - Na zimevuka mipaka nafsi za waovu wasio Waarabu.*

*Ofisi ya mfalme kisra imevunjika - Kutokana na msituko wa haki wala si msituko wa kufika kwake.*

*Ulikuja na watu wakiishi hovyo haupiti kwao. Isipokuwa sanamu ipo jirani na sanamu.*

*Na ardhi imejaa waovu na kurahisisha. Kwa kila muovu wa viumbe ni mwenye kutawala.*

*Na watu wenye nguvu wanawadhulumu wanyonge wao - Kama vile simba kwa wanyama na papa kwa samaki wengine.*

*Mwenyezi Mungu amekusafirisha usiku ambapo Malaika wake - Na Mitume wake wapo Msikiti uliombali wamesimama.*

*Alipowafikia wamemzunguka kiongozi wao - Kama vile nyota kwa mwezi au kama vile askari kwenye pendera.*

*Waliswali nyuma yako kila mwenye upendo - Na mwenye kufaulu kwa kipenzi cha Mwenyezi Mungu anaswali nyuma yake.*

*Umepanda mbinguni au zaidi ya hapo - Kwenye kizazi chenye nuru ya utukufu.*

*Kipando cha fahari na heshima kwa ajili yako. Siyo kama farasi wa kawaida wala hata mwenye nguvu na uzuri.*

*Matakwa ya Muumba na utengenezaji wake - Na uwezo wa Mwenyezi Mungu upo mbali na shaka na tuhuma.*

*Mpaka umefika kwenye mbingu isiyofikiwa kwa kuruka - Wala kufikwa kwa kutembea.*

*Na ikasemwa kila Nabii yupo katika cheo chake - Na ewe Muhammad hii ni Arshi basi ipokee.*

*Ukaweka elimu ya dini na ya dunia - Ewe msomaji wa kitabu bali ewe mshika kalamu.*

*Umejua siri kati ya pande mbili hizi na kufahamu - Hazina ya elimu na hekima.*

*Waulize kikundi cha washiriki waliozunguka pango - Lau isingekuwa kuondolewa basi usingetajwa.*

*Je wameona athari ya muangaza au wamesikia - Sauti ndogo ya kumtakasa Mola ama upole wa sauti ya Qurani.*

*Na je umekuwa utando wa buibui kwao - Ni kama msitu na mimea na miti midogo kama vile imesongamana.*

*Wakarudi na nyuso na ardhi zikiwalaani - Kama vile batili mbele ya utukufu wa haki inavyoshindwa.*

*Lau usingekuwa msaada wa Mwenyezi Mungu kwa wawili hao wasingesalimika - Na jicho lake pembezoni mwa nguzo ya dini halikusimama.*

*Wakakingwa na Mwenyezi Mungu na wakajistiri - Na mwenye kuhifadhiwa na Mwenyezi Mungu hafunikwi na mwengine.*

*Ewe Ahmed kwangu ni fahari kwa kujiita jina hilo - Ni namna gani nisijiite kwa jina la Mtume.*

*Wanaokusifu wote na wanaokupenda wanamfuata - Mshairi na mtunzi mzuri wa kale.*

*Kukusifu kwetu kunatokana na upendo halisi - Na upendo wa kweli unamsifu mkweli wa maneno.*

*Mwenyezi Mungu anashuhudia kuwa mimi simpingi - Ni nani mwenye kuweza kupinga haki.*

**Na anasema tena:**

*Wewe ni zaidi ya mwezi kwa uzuri na ubora - Na zaidi ya bahari katika kheir na ukarimu.*

*Ukilingananishwa na mlima basi mlima utapungua - Na nyota zinazotoa nuru ukilinganishwa nazo utazizidi kwa nuru yako.*

*Ni zaidi ya simba katika uthibiti wake - Pindi unapokwenda kumsaidia asiye na silaha anakuwa shujaa.*

*Umetajwa pamoja na yatima katika Qurani ikiwa ni kumkirimu - Na thamani ya lulu iliyohifadhiwa iko kwa yatima.*

*Mwenyezi Mungu amegawa riziki kati ya watu - Na wewe umepewa hiyari katika riziki na mgao.*

*Ikiwa kwenye jambo utasema ndio au hapana. basi ni hiyari ya Mwenyezi Mungu kwako kusema hapana au ndio.*

*Ndugu yako Isa aliomba na maiti ikamsimamia - Na wewe umehuisha vizazi vilivyokufa.*

*Wakasema wewe umepigana vita na Mitume wa Mwenyezi Mungu hawakuletwa - Ili kuuwa nafsi wala hawakuja kumwaga damu.*

**Anaendelea kusema:**

*Ewe Mola watu wengi wamehuishwa kutoka kwenye kifo - Na uma nyingi wameamka kutokana na usingizi usio na faida.*

*Furaha na nuksi na ufalme wewe mmiliki wake - Unabadilisha kati ya shari na heri.*

*Hukumu yako kati yetu tunairidhia - Wewe ni Muadilifu katika hukumu na wewe unalipiza kisasi.*

*Basi tufanyie huruma kwa ajili wa Mtume wa watu wote - Na usiwazidishie watu wake adhabu wala maangamizi.*

*Ewe Mola wetu umefanya vizuri Waislamu kuanza naya - Basi ukamilishe ubora huu kwa mwisho mwema.*

*Sehemu ya tungo ya ulizeni moyo wangu ya Ahmad Shawky:*

*Imeonekana kuzaliwa kwa Mtume na kuenea furaha yake - Kuzaliwa mijini na majangwani.*

*Na binti Wahbi amezaa kwa ulimwengu - Mkono mweupe umezunguka shingo.*

*Amemzaa na akiwa na nuru yenye kutoa mwangaza - Kama vile mbingu zinapozaa nyota.*

*Paa la nyumba limekuwa na nuru - Inayoangaza milima ya Makka na maeneo mengine.*

*Madina imesahauliwa na Makka imejazwa harufu nzuri - Na kutoa harufu na kuwa nzuri.*

*Baba wa Zahra nimepita uwezo wangu - Kwa kukusifu wewe kwa kiasi cha mimi kunasibishwa kwako.*

*Na hakuna msomi anayejua Ufasaha vizuri - Ikiwa hatokuzingatia wewe kwake ni kitabu.*

*Nimewasifu wafalme na cheo changu kimezidi - Na pindi nilipokusifu wewe mawingu yamefuatilia.*

*Nilimuomba Mwenyezi Mungu kwa watu wa dini yangu - Ikiwa ni njia kwangu anajibu.*

*Na hakuna kinga kwa Waislamu isipokuwa Wewe - Yanapowafika madhara wanarejea kwako.*

*Kana kwamba nuksi pindi ilipowafikia - Kunguru wakaruka katika miji yote.*

*Lau wengefuata njia yako ingekuwa nuru kwao - Na ingekuwa ni zuio la hiyo nuksi.*

*Umewajengea nguzo iliyotokana na maadili - Na wakaiacha nguzo wakaporomoka.*

*Na walikuwa hawafuati maadili - Na maadili ni bora yafuatwe na yaheshimiwe.*

*Bila ya maadili basi simba angekuwa sawa na mbwa mwitu - Na mwenye nguvu na haki akawa mnyonge.*

*Na ukillinganisha maadili mema na elimu - Basi elimu itanyenyekea mbele ya maadili.*

***

## Miongoni mwa tungo za Imamu Al-Buswiry:

*Muhammad ni Bwana wa wanadamu na majini mbingu na ardhi - Na pia kwa Waarabu na wasokuwa Waarabu.*

*Mtume wetu anayeamrisha na aneyekataza hakuna yeyote - Ambaye ni mpole kuliko yaye anapoamrisha au anapokataza.*

*Yeye ni kipenzi ambaye uombezi wake unategemewa - Kwa hali zote nzito miongoni mwa hali ngumu za watu.*

*Alilingania kwa Mwenyezi Mungu basi wenye kushikamana naye - Ni wenye kushikamana na kamba isiyo katika.*

*Amewazidi Manabii katika kuumbwa na katika maadili - Na Manabii hawakumkaribia katika elimu wala ukarimu.*

*Na wote hao kwa Mtume ni sehemu tu - Kama kijiko cha maji ya bahari au tone la mvua.*

*Na wan*asi*mama kwake kwa hali yao - Ni kama sehemu ndogo katika elimu yake au kama neno katika hekima zake.*

*Yeye ndiye ambaye sura yake na maana yeke vilikamilika - Kisha ameteuliwa kuwa mpendwa mwenye sura ya ukamilifu.*

*Ameepukana na wakufanana naye katika mazuri yake - Na kiini cha sifa njema ndani yake hakigawiki.*

*Acha walichokisema Wakristo kwa Mtume wao - Na hukumu utakavyo kwa kumsifu na lete hakimu.*

*Na jinasibishe kwake kwa heshima uitakayo - Na jinasibishe kwenye uwezo wake kwa utukufu uutakao.*

**Anaendelea kusema:**

*Hakika ubora wa Mtume wa Mwenyezi Mungu hauna mpaka - Wa kuelezewa na mdomo wa mtamkaji.*

*Lau ukilinganisha cheo chake alama zake ni kubwa - Jina lake litukuzwe pindi anapoitwa mwalimu wa kutengeneza vilivyoharibika.*

*Hajafanyiwa mitihani katika mambo yanayoeleweka na akili - Kwani anatutaka tusiwe na shaka na kudanganyika.*

**Akaendelea kusema:**

*Mola wetu tukirimu kwa kuumbwa kwa Nabii aliyejipamba na tabia njema. Mwenye kuleta bishara furaha na sifa nzuri.*

*Ni mfano wa maua wakati wa kuchanua kwake na mwezi wakati wa kukamilika. Na bahari katika ukarimu na zana katika umuhimu wake.*

*Hakuna harufu nzuri kuliko sehemu alipozikwa Mtume - Amefaulu kwa anayesikia harufu nzuri ya kaburi lake.*

**Anasema tena:**

*Kuzaliwa kwake kumeeleza utukufu wa kuumbwa kwake - Ewe mwema wa mwanzo wake na mwisho.*

*Siku ambayo Wafursi wamesikitika sana kwani - Wameonywa na kuwaletea madhara na majanga.*

*Na amelala mfalme wa kisra na chombo chake kimevunjika - Kama vile watu wa kisra wanatofautiana na hawakubaliani.*

*Moto ulizimika kwa pumzi za wamtaka msamaha - Mto pia watoa maji mengi kwa sababu ya furaha ya kuzaliwa kwake.*

*Na watu wa mji wa saawah wamesikitika kukauka kwa maji ya ziwa lao - Na anayekuja kwa ajili ya kunywa amerudi akiwa amekasirika.*

*Kana kwamba moto umeloweshwa maji - Kwa huzuni na kwa maji haukuwa moto wenye uwezo wa kawaka.*

*Na majini wanazima na nuru ni yenye kuchomoza - Na haki inaonekana kwa maana na kwa maneno.*

*Kwa ulinganio wake miti imekuja ikiwa yenye kunyenyekea - Inamuendea kwa ugoko bila ya nyayo.*

*Kana kwamba umechora mstari kwa yale uliyoyaandika - Matawi yake yanatokana na hati nzuri katika kuandika.*

*Mfano wa mawingu yaliyokuja yakitembea - Yanamuokoa na hali ya joto kwa msafiri hulindwa.*

*Na kilichomo pangoni miongoni mwa heri na ukarimu - Na macho ya makafiri kwake yamekuwa na upofu.*

*Mkweli yumo pangoni na rafiki - Na wao wanasema pangoni hakuna yeyote.*

*Wakadhani kuwa njiwa na buibui kwa - Mbora wa viumbe hawezi taga wala kufumo utando.*

*Ulinzi wa Mwenyezi Mungu umekuwa - Ni zaidi ya ngao na ukuta mkubwa.*

*Na zama zinaniumiza na kuomba msaada - Isipokuwa nimejikuta nipo jirani yake.*

*Na wala sikuomba utajiri wa dunia na akhera kupitia yeye - Isipokuwa nimepokea kutoka mbora wa kupokea.*

*Usikanushe ufunuo kuuona kwake kwani yeye - Ana moyo pindi macho yanapolala moyo haulali.*

*Alama za Haki kutoka kwa mwingi wa Rehma zenye kusema - Hapo zamani sifa za mwenye kusifika kwa ukale.*

❊❊❊

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| Utangulizi | 5 |
| Utafiti wa Kwanza: Mazungumzo ya Quran kuhusu Mtume S.A.W | 15 |
| Utafiti wa Pili: Umuhimu wa Sunna Takatifu na nafasi yake katika utungaji Sharia. | 35 |
| Utafiti wa Tatu: Mtume wa Utu na Ubinadamu. | 69 |
| Utafiti wa Nne: Kumpenda Mtume wa Mwenyezi Mungu | 85 |
| Ni sehemu isiyogawanyika katika Imani. | |
| Utafiti wa Tano: Kuwa na adabu na Mtume wa Mwenyezi Mungu | 97 |
| Utafiti wa Sita: Matendo ya Mtume SAW katika kuendesha nchi. | 107 |

Utafiti wa Saba: Baadhi ya mashairi katika upendo na ubora 115

wa Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W

Mashairi ya Ahmad Shauqy katika kumsifu Mtume

Shirika Kuu la Vitabu la Misri.

Msimamizi wa miradi ya kitamadani.

**Marwan Hammad**

Mkaguzi

**Faryal Fuad**

Mtangenezaji wa jarada la

**kitabu Muhammad Baghadady**

Upande wa Ufundi

**Mervat Antar An-Nuhas**

Upande wa Ufundi Mirfat Antar An-Nuhas

ISBN